amepiga simu namba 112. Kutoweka kwa mtoto jina lake Francesco Rubino mwenye umri wa miaka tisa hivi, kulikuwa kumeshtakiwa. Basi, ile simu ilitoka kwa babu yake mtoto. Yule mtoto alizoea kupita wakati wa likizo kwa babu yake kwa sababu, nadhani, wazazi wake waliachana".

"Sawa Luteni, acha habari za mambo yasiyo na maana. Sema kuhusu mambo ya muhimu tu, tafadhali".

Luteni alitaka kujibu kwa vyo vyote. Alikuwa hajapenda kikomo kile. Walakini yeye alikuwa askari na, kwa hiyo, hakusema neno na baada ya muda mfupi sana alianzisha tena shuhuda lake.

"Nilipopokea ile simu kutoka kwa opereta nilituma doria la askari kiungani kwa babu…".

"Na kiunga kilikuwa wapi?".

"Nilikuwa nikikuambia, kiunga cha babu kilikuwa… kiko mtaani panapoitwa Capitolo karibu na hamamu inayoitwa 'Duna Beach'. Jamii ya watu wa doria walipofika kule na mbele ya babu yake mtoto, wakatambua kwamba labda tukio lingeweza kuwa la maana sana yaani yule mtoto akatoweka karibu saa mbili, kwa hiyo wakawasiliana nami. Baadaye nilimjulisha mshiriki wa kituo cha polisi ili washirikiane wao pia na upelelezi na halafu nilienda pale pamoja na watu wa kundi la opereta".

"Na upelelezi ulitengenezwaje?".

"Zaidi ya polisi wa kiserekali, askari polisi walivutwa pamoja, kwa ufupi, polisi wa munisipali. Bila shaka niliwajulisha wakuu wangu wa mjini Bari. Lazima niseme kwamba kapteni alikuwa likizoni kwa sababu alikuwa mgonjwa na mimi nilikuwa mkuu wa kundi la askari la Monopoli. Kwa kila hali, baada ya upelelezi wa kwanza, askari wa kutoka mji mkuu wa wilaya walishiriki uchunguzi. Asubuhi yake tuliwaita wale askari wanaotenda kazi kwa msaada wa mbwa.

"Je, baada ya mwingilio wa mbwa yalitokea mambo?".

"Ndiyo bwana. Sisi tuliwapelekea mbwa kiungani kwa babu, na tulifanya mbwa waanzishe moja kwa moja toka mahali ambapo mtoto alikuwa amecheza alipoonwa mara ya mwisho. Mbwa walianza kazi yao kwa moyo, walisaka kiwanja kizima – kilichokuwa nje ya mlango wa kiunga – wakafika kijia cha ndani kinachoanza toka barabara ya Capitolo mpaka ile *compound*, wakakimbia kwa kile kijia mpaka barabarani na halafu wakasimama. Tuseme kwamba mahali ambapo barabara na kile kijia vinakatana, wale mbwa walipotea nyayo za mtoto yule. Tuliwapelekea mbwa upande wa njia, halafu mita mia ng'ambo ya huku



na ya pili lakini bure. Mahali pa mwisho, ambapo mbwa walionyesha kusikia gugumu ya mtoto, palikuwa barabara na kijia vinapokatana. Kwa hiyo tulifikiri kwamba yule mtoto alikuwa amepanda gari".

"Na yule mtoto alikutwa lini? Na kwa jinsi gani?".

"Ndiyo, tuliyakuta maiti ya mtoto karibu na Polignano, katika shimo la kutekea maji lililokuwa mashambani karibu na pwani. Tulipokea simu ya siri kituoni kwa polisi mjini Polignano".

"Alisema nini yule aliyepiga simu?".

"Alisema kwamba mtoto ambaye tulikuwa tukimtafuta alikuwa katika shimo la kutekea maji lililokwapo mahali pa San Vito, katika jimbo la mji wa Polignano. Alieleza wazi shimo hili lilikuwa wapi, nina maana alisema maneno kama: shimo ni karibu na kilometa… sasa sikumbuki kilometa ngapi. Kwa kila hali alitaja barabara namba 16".

"Je, unaweza kutuambia kama mtu huyu alisema kwa tamko la peke yake…".

Ulifika muda wa kuutia utetezi.

"Samahani Mheshimiwa. Kwa sasa nitaacha kwamba simu ile ilikuwa ya siri na nitakufahamisheni kwamba Luteni, kama ninavyojua mimi, hakupokea simu yeye mwenyewe. Nafikiri kwamba maswali kuhusu aina ya simu ile – iwapo yaruhusiwe, lakini kuhusu mambo haya tutazungumza baadaye – lazima mwulize mwanapolisi aliyepokea simu".

Mwenyekiti alisema kwamba nilikuwa na haki na hakukubali swahi hilo. Maulizo yaliendelezwa kwa jinsi ya kukinaisha kuhusu maendeleo ya upelelezi hata Abdou alipokamatwa. Yule Luteni alikuwa ameusawazisha upelelezi tu bila kushiriki upekuzi wala kuwajadili mashahidi wa muhimu na, kwa maoni yangu, yule alikuwa mtu asiye aula.

Cervellati alipomaliza kusema, wakili wa jamii alisema kwamba maulizo yaliyoendeshwa na Mwendesha mashtaka yalikuwa ya kuridhisha na, kwa sababu hii, yeye hakuwa na maswali mengine.

Mwenyekiti wa Mahakimu alisema kwamba sasa hivi zamu yangu ya kusema imetimia.

Kwa kweli, maswali yangu ya kumwuliza Luteni yalikuwa machache sana na ningaliweza kuyarukia maulizo yangu. Lakini ilikuwa lazima wale wa baraza la wazee wa mahakama wafahamu kuweko kwangu. Kwa sababu hii nilikubali kumjadili shahidi.

"Haya Luteni, wewe umesema kwamba ile simu ya kushtaki mtoto alikuwa ametoweka ilipigwa saa…".

"Saa mbili kasoro dakika kumi".

"Saa mbili kasoro dakika kumi, asante. Lakini doria ya askari uliyotuma wewe walifika lini kiungani kwa babu mtoto?"

"Walitumia muda wa kufaa kufika Capitolo kutoka kituo cha polisi cha Monopoli, yaani robo saa au dakika ishirini".

"Na mtoto alitoweka saa ngapi?".

"Siwezi kujua saa halisi…".

"Angalia Luteni, nimekuuliza swali hilo kwa sababu wewe ulipomjibu Mwendesha mashtaka umesema kwamba askari walitambua kwamba mtoto alitoweka kabla ya saa mbili".

"Bila shaka, nina maana askari wangu walinijulishia mambo".

"Tafadhali, sasa uiambie korti na kwa habari ulizo nazo, karibu saa ngapi mtoto alitoweka?".

"Kama nilivyokuwa nimeshakuambia, mtoto alitoweka kabla ya saa mbili".

"Kwa hiyo?".

"Karibu saa kumi na mbili".

"Mtoto alitoweka karibu saa kumi na mbili na babu yake alipiga simu saa mbili kasoro dakika kumi, sawa?".

"Ni taratibu za kuonya".

"Ndio, tuseme kwamba mtoto alitoweka saa kumi na mbili na babu yake amepiga simu saa mbili kasoro dakika kumi. Sawa?".

"Ndiyo".

"Mmemwuliza babu kwa sababu gani alisubiri zaidi ya saa mbili kabla ya kupiga yowe?".

"Sijui kwa sababu gani alisubiri. Labda walijaribu kumtafuta…".

"Samahani ikiwa nakudakiza bwana Luteni. Mi sikuuliza maoni yako. Niliomba usimulie ikiwa babu alisema kwa nini alisubiri karibu saa mbili. Unaweza kunijibu?".

"Sikumbuki kama alisema".

"Na wewe unakumbuka kama ulimwuliza?".

"Hapana, sikumbuki".

"Kwa hiyo ni sawa kusema kwamba wewe hujui ilitokea nini wakati wa zile saa mbili zilizopita kati ya kutoweka kwa mtoto na simu ile".

"Sikiliza, wakili, wakati ule sisi tulijitahidi kumtafuta mtoto na kutunga matendo na kadhalika, na hatukufikiri kabisa kuelewa kwa sababu gani babu yake mtoto alikuwa amechelewa kushtaki, iwapo



alichelewa".

"Ndiyo, hakuna mtu anayetaka kushindana kwa maneno kuhusu usawa wa kazi yenu. Nataka kukuuliza maswali mengine. Kabla Mwendesha mashtaka hajakudakiza, wewe umeonya kwamba wazazi wake mtoto waliachana…".

Mwendesha mashtaka alinidakiza.

"Samahani Mheshimiwa, lakini nafikiri kwamba mambo kama talaka ya wazazi wake mtoto ndio mambo yasiyolingana na hoja ya mashtaka…"

Cotugno pia alijitia kati.

"Kama wakili wa jamii, nashiriki ubishi. Watu wa famiglia ile wameshaona majonzi kwa msiba na hatujui kwa sababu gani mambo yao binafsi yamevurugwavurugwa".

Kwa kawaida ningenyamaza. Nilikuwa nimetoa swali hii kwa kuelewa vizuri zaidi na kwa sababu Mwendesha mashtaka alikuwa amemdakizia Luteni jambo lile. Lakini sasa niliona kwamba hisia za washindani wangu zilikuwa za kupita kiasi. Kwa hiyo nilifikiri afadhali nisisitize tena juu ya mambo yale, ili niweze kuelewa itatokea nini.

"Mheshimiwa, mi nimeshindwa kuelewa hisia za Mwendesha mashtaka na za Wakili wa jamii kuhusu mambo haya. Sipendi kunyetea famiglia yake mtoto na majonzi yao. Lakini sioni kama swali langu lingeweza kupenya moyoni hivyo. Maana yangu ya pekee ni kuelewa vizuri ilitokea nini muda uliofuata kutoweka na ikiwa wazazi wake mtoto walishiriki kumtafuta".

"Sawa, unaweza kuendelea".

"Asante, mheshimiwa. Basi, tulikuwa tukizungumza kuhusu wazazi wake mtoto ambao walitengana ndoa – au wameachana – si ndio?".

"Ndiyo, nafikiri".

"Na hali zilivyo, ulijua lini?".

"Nilipokuenda kule".

"Wazazi wake mtoto walikuwa kule?".

"Hapana".

"Unajua walikuwa wapi?".

"Sio, yaani nafikiri mama yake alikuwa nje kwa likizo na babake sijui alikuwa wapi".

"Ulijuaje habari hizi?".

"Nilijulishwa na mzee Abbrescia, yaani babu mzaa mama mtoto, nilipofika kule".

"Na mzee Abbrescia alikuambia kwamba wazazi wake mtoto walikuwa wameshajulishwa kutoweka?".

"Ndio, aliniambia kwamba alikuwa amemkuta mwanake kwa simu ya mkononi na yule bibi alikuwa akirudi nyuma, sasa sikumbuki toka wapi. Au labda hakuniambia kabisa. Kulahali jioni, yaani usiku nilimwona mama yake mtoto kiungani ambako sasa ni kituo chetu kwa upelelezi".

"Na baba yake mtoto?".

"Sikiliza, kuhusu baba mi habari sinazo. Nilimwona bwana Rubino kesho yake, lakini sijui amefika lini na toka wapi".

"Unajua kama yeye pia alikuwa likizoni?".

"Sijui".

"Unajua kama babu na bibi wazaa mama mtoto walimwita baba mtoto pia?"

"Sijui".

"Kwa ufupi, unajua baba mtoto alijulishwa na nani?".

"Hapana".

"Kwa kila hali, jioni mtoto alipotoweka, mama mtoto ameshafika na baba mtoto bado. Sawa?"

"Sawa".

"Asante, sina mengine".

Kwa kweli, maswali niliyotoa yalikuwa bure. Utengano wa wazazi wake mtoto ulikuwa mbalimbali na kutoweka kwake na hoja ya mashtaka na yote mengine. Labda Mwendesha mashtaka na Wakili wa jamii walikuwa na haki waliposhindana na yale maswali yangu.

Lakini nafasi yangu ilikuwa ndogo. Kabisa. Kwa hiyo ilikuwa lazima nifanye kitu fulani, na hata bila kufikiri kwanza, ili nipate mwelezo na kuelewa njia ya kupitia ilikuwa wapi, yaani njia ya kujaribu kupitia. Kwa vitabu vya mwongozo kwa wanasheria mwenendo wangu ni mbaya.

Imeandikwa kwamba haifai kutoa maswali ambayo huwezi kujua mbele majibu yatakayokuja. Halafu, haifai kuhojihoji bila kuwa na mradi wa kupatia. Lazima maulizo yapangishwe na huwezi kutunga papo hapo kwa sababu ungeweza kuthibitisha uwezo wa mshindani wako. Na kadhalika, kadhalika na tena kadhalika.

Ningependa kuwaona wale mabwana wanaoandika vitabu vya mwongozo wakati wa mashtaka magumu kama haya. Nataka kuwaona kati ya makelele na uchafu, tena kati ya damu na mavi, yaani kati vyote vinavyoainisha mashtaka ya kweli. Na nataka kuwaona wakati



wanapotekeleza nadharia zao.

Huwezi kuhojihoji kama huwa na mradi wa kupatia.

Ningependa kuwaona. Ilinibidi nifuate mwendo huu bila kupanga kitu na sio mashtaka tu.

Mashahidi wengi walisikilizwa katika baraza lile. Alifika yule mwanapolisi aliyepokea ile simu ambayo kwa ajili yake iliwezekana kuyakuta maiti ya mtoto. Alisema kwamba yule mtu wa siri aliyepiga simu alikuwa na tamko *geni*. Mwendesha mashtaka alitaka kujua habari zaidi. Labda angalipenda shahidi aseme kwamba tamko lile lilikuwa la *kisenegali*. Lakini yule mwanapolisi hakusaidia sana. Kwa maoni yake, tamko lile lilikuwa geni tu. Lakini elezo hili halikuwa na maana.

Walisikilizwa wale wanapolisi wanaosaidiwa na mbwa kwa kazi yao na hawa pia hawakusimulia jambo jipya zaidi kuliko yalihadithiwa na Luteni. Alifika pia yule mzima moto aliyeshuka shimoni ili afunge kwa kamba kusudi kuinulia mwili wa mtoto. Shuhuda hili lilikuwa la huzuni na tena bure.

Halafu tulisikiliza wengi wa wazoefu wa hamamu ya 'Duna Beach'. Walikuwa wanamjua Abdou, wengine walikuwa wamenunua bidhaa zake na wote walikumbuka kwamba mara nyingi yule Msenegali alisimama kuzungumza nao pwani. Walisema kwamba mara nyingi walikuwa wamemwona akizungumza na mtoto mfu. Niliwauliza kama Abdou alivyokuwa ametenda na wote walisema kwamba huambilika na hakuwa na mtazamo usio wa kawaida. Tena, yeye na mtoto walionekana kuwa marafiki.

Ingekuwa afadhali tungalimsikiliza daktari ya kisheria aliyefanya uchunguzi wa maiti, lakini alikuwa hayupo. Alituma hati ya kuonya haki na aliomba asikilizwe baraza lijalo. Mwenyekiti wa Mahakimu alikuwa mwenye furaha kuondoka mapema kidogo. Mashtaka yalirejeshwa kwa jumatatu ijayo.

Nilifikiri kwamba wakati ule, bahati mbaya, utakuwa wakati wa joto sana. Hatuwezi kuwa na bahati kwa hali ya hewa mwezi wa sita.

# 5

Wiki mbili zilipita tangu usiku ule nilipokuwa nyumbani pa Margherita. Tangu usiku ule hatujawahi kuonana au kuwasiliana. Labda kwa sababu kesho yake asubuhi ilinitokea jambo lisilo la kawaida yaani nilijisikia kama nimo kosani kwa Sara. Nilifikiri hivyo.

Lilikuwa jambo lisilo la kawaida kwa sababu Sara alikuwa ameniacha yeye na tangu mwaka moja na nusu mbele alikuwa ameanza kuishi maisha yake ya binafsi. Walakini, kwa upuuzi, kwa mara ya kwanza nilihisi kama nilimsaliti. Kwa sababu nilikuwa vizuri sana pamoja na Margherita usiku ule uliopita.

Wakati wa ndoa yetu, yaani tulipoishi pamoja, mi nilitenda vibaya sana. Na matendo yale niliyofanya yameniingia na dharau kwangu, yaani yamenifanya nisiwe na raha. Lakini, kwa kusema kweli, sikujisikia kosani kama baada ya usiku ule.

Nimelifikiriafikiria jambo lile. Wakati ule sijawahi kufahamu. Labda sasa nimeelewa.

Watu huzoea kupenda mambo yanayohusiana na huzuni, hasa na mkato wa tamaa. Kila tulipotendewa na mtu fulani, huzuni inapotaka kumaliza, sisi tunapagawa na hofu. Labda kwa sababu tunafikiri kwamba kila kitu kinamaliza.

Sio kweli, lakini bado sijakuwa tayari kuelewa.

Na sikumwita Margherita. Sikumtafuta kwa sababu nilikuwa na hofu ya kupotewa na huzuni yangu. Kwa kweli, sisi binadamu wa ajabu.

Kwa kila hali, aliniita yeye. Mi nilikuwa maktabani, saa nane na nusu baada ya mchana, saa ile mi naipenda sana. Maktabani hakuna watu, kwa hiyo inawezekana kusikiliza muziki na, kama pasipo na watu, inawezekana harufu ya karatasi hewani.

Nilipoitikia simu ya mkononi, nilikuwa nikisoma insha haraka haraka kama nilivyojifunza wakati ambapo sikuwa na pesa za kutosha kwa kuvinunua vitabu nilivyopenda.

Nilikuwa nikifanya nini? Ah, nilikuwa maktabani. Nipende kunywa kahawa pamoja naye? Ndio. Nipe muda wa kufika nyumbani kutoka maktaba ya "Laterza". Muda kama dakika kumi tu. Hapana, ndio sawa kahawa ya kawaida. Tutaonana mapema. Ndio, mimi pia nafurahi kukusikia. Kweli.



Wakati wa kufululiza mwendo – bila kutambua – kuelekea nyumbani nilifikiri kwamba sijakumbuka nilimpa namba ya simu yangu ya mkononi; tena sijakumbuka nilimwambia matatizo yangu kwa usingizi na kuhusu kahawa niliyopendelea; na kwamba mwito wake ulinifurahisha.

Alinipokea akinipa mkono, na akinivutia karibu naye kidogo na kunibusu mara mbili mashavuni. Ilikuwa salamu ya kirafiki, hivi kama mwenzi. Walakini nilisikia kitu fulani chini ya kitovu changu na niliona haya, kidogo tu.

Alinistarehesha roshanini palipokuwa upande wa kaskazini na kwa hiyo palikuwa kivulini na penye ubaridi. Tulikunywa kahawa na tulianza kuvuta sigara. Yeye alivaa suruali za aina ya 'jeans' zenye rangi ya samawati, na shati jeupe lenye maandiko haya: *what the caterpillar calls the end, the rest of the world calls a butterfly. Lao Tze.*

Ngozi ya uso wake na ya mikono ilikuwa nyekundu kwa joto la jua. Mikono yake ilikuwa mizuri na yenye misuli. Alikuwa amesoma gazeti lililozinyonya habari juu ya kesi ya Abdou. Alikuwa amesoma kwamba mimi nilikuwa mtetezi wake Abdou na alinipigia simu kwa hiyo, yaani kwa sababu alitaka kujulishwa zaidi. Nilijisikia kama ninaumwa kidogo. Alikuwa amenipigia simu ili ajue zaidi kuhusu kesi tu, kwa sababu alikuwa mpekuzi tu. Kwa dakika moja tu, nilifikiri sitamjibu. Lakini, kwa bahati nzuri, nilisema.

Nilimwambia zote. Yaani, habari kuhusu maandiko ya upelelezi yaliyoonyeshwa na Mwendesha mashtaka, kwamba ile ilikuwa kesi ya aina ya kituhuma, tena yenye tuhuma *nyingi*; jinsi ambavyo nalipatiwa kazi ile, kila kuhusu Abagiage na kila kitu.

Swali nililosubiri, limefika.

"Na wewe unafikiri kwamba kijana huyu Msenegali hana hatia?"

"Sijui. Kwa upande mmoja sio tatizo langu mimi. Inatubidi kuwatetea vizuri iwezekanavyo, kama wasiokosa au wana hatia. Mahakimu tu wanalazimishwa kuupata ukweli kama uko. Sisi tunapaswa tuwatetee washtakiwa".

Alianguka kucheka.

"Hongera. Ilikuwa nini? Labda ni utangulizi wa kozi wa *Ushuhuda wa mwanasheria*? Una nia ya kuwa mwanasiasa?".

Nilitafutatafuta jibu la kufaa bila kulipata. Alikuwa na haki na mimi nimejiuliza kwa sababu gani nilikuwa nimesema kwa kiburi kile cha kuchekesha.

"Je, si umechukizwa kwa maneno yangu? Mi nimechezacheza tu".

Aliniangalia usoni akinyosha koo, akikaribia upande wangu na mimi nilitambua kwamba nilikuwa nimebaki kimya kwa muda.

"Ni kweli, nilikuwa mcheshi. Mi nafikiri kwamba Abdou hana hatia, lakini naogopa kusema".

"Kwa nini?".

"Kwa sababu nafikiri hivyo kufuatana na utambuzi wangu, na fikra zangu. Mi nampenda na, kwa hiyo, nafikiri hana hatia. Kwa sababu *ningependa* asiwe na hatia. Halafu, naogopa atahukumiwa. Nikisadiki sana na yeye atahukumiwa – kwa sababu inawezekana atahukumiwa – nitasikitika sana. Lakini, bila shaka, yeye atasikitika zaidi".

"Kwa nini unampenda?".

Nilishangaa sana nilipomjibu bila kufikiri. Na tena, nilipopata jibu wakati ule ule niliposema:

"Kwa sababu ananikumbusha kitu fulani ninacho ndani yangu, nafikiri".

Ilionekana kwamba jibu langu lilimtia moyoni, kwa sababu alibaki bila kusema neno, kwa macho chini, upande wa kushoto. Alikuwa akitafutatafuta kati ya vitu vyake, nilifikiri. Nilibaki kumtazama mpaka amemaliza, mpaka alianza tena kusema.

"Ningependa kuja kuiona kesi. Naweza?".

"Ndiyo, unaweza. Baraza lijalo litakuwa siku ya Jumatatu".

Nilitabasamu, sijui kwa sababu gani. Sijui kwa nini, nilifikiri kwamba hakulikosa pigo moja. Nilifikiria vitabu vyake vya mieleka vilivyokuwa rafani pake. Bado sijamwuliza kwa sababu gani alikuwa navyo, na kama akifanya mazoezi ya mwili ya aina gani. Nilimwuliza sasa.

"Unaweza kuzisoma utakapotaka. Mi nitaweza kuzileta hapa, lakini labda itakuwa afadhali ukija ofisini mwangu. Karatasi nyingi kweli. Kwa nini una vitabu vile vingi vya mieleka?".

"Mi nafanya 'aikido' kidogo. Tangu nilipoacha kunywa vinywaji".

" 'Kidogo', maana yake nini?".

"Mimi nipo daraja la 'dan ya pili', manda mweusi".

"Ningependa kukuona huku unafanya mazoezi".

"Sawa. Njoo ndani".

Tulirudi ndani, alichukua boxi moja toka kabatini, aliwasha kirekodi cha mkanda wa video na aliniambia niketi.

Mkanda ule ulianzishwa kwa onyesho la kituo cha mazoezi ya mwili



cha kijapani, kisicho na watu na chenye 'tatani' ya rangi ya majani.

Sauti moja imesikika lakini maneno yaliyotolewa mi sijayaelewa, kisha, msichana aliyevaa 'kimono' nyeupe na suruali pana nyeusi alionekana. Nywele zake zilifunika nyuma ya kichwa chake. Baada ya sekunde chache nilimtambua Margherita. Macho yake yalikuwa yakitazama upande wa nje. Toka upande ule mwanamume mmoja aliingia. Yeye pia alivaa mavazi yale yale. Alimshika kwa koti; msichana alimshika kwa mkono na alichora kama duara kwa miguu yake. Ilionekana kama kwamba alikuwa akijimudu kwa uelegevu, lakini vile vile sijaelewa vizuri kwa jinsi gani yule mwanamume alikuwa akitupwa kwenye 'tatani' kwa mchakarisho. Lakini hakusimama na akizungukazunguka na kuinua tena na kugeuka, alimshambulia tena Margherita na aliangusha mkono wake juu ya kichwa cha msichana. Kwa zunguko jipya na mwendo usioeleweka, yule mwanamume alikuwa akiruka tena angani, na suruali zake pana na nyeusi zilikuwa zikichora michora mizuri. Katika maonyesho mengine yaliyofuata, washindani wale wawili walikuwa wakipigana kwa fimbo na visu.

Tamasha ile iliyodumu kwa dakika ishirini hivi, ilikuwa ya hiponozi. Kisha Margherita aliutoa manda na aliurudishia mahali pake. Alikuwa amebaki bila kusema neno wakati wote. Nami pia. Na baadaye tuliendelea kuwa kimyani kwa muda isiyoelezwa. Walakini tena labda kwa mara ya kwanza maishani mwangu, nilijiona vizuri katika ile hali ya kimya. Nilikuwa sijaona hangaiko la kujaza, kwa jinsi fulani, kwa sauti yangu au kwa tutumo. Niliona kama nilishinda kupata uzuri wa ile hali ya kimya. Muziki yake, nilifikiri, katika muda ile.

Nilipotaka kuondoka, nilitambua kwamba kwa wakati ule wote, kabla na baada ya filamu ile, nilikuwa nimeitazama mikono yake. Nilikuwa nimeitazama ngozi yake ya rangi ya dhahabu na yenye nuru; na misuri yake mirefu na yenye nguvu. Nilikuwa nimeyatazama malaika ya rangi ya kitani mikononi pake na tena yalivyosimama wakati upepo ulipokuja kule roshanini.

"Mikono yako mizuri sana". Nilimwambia tulipokwishafika mlangoni. Halafu, nilifikiri kwamba haiwezekani mambo yaivie kama kawaida yangu. Kwa hiyo nilikamilisha.

"*Wewe* mwanamke mzuri sana".

"Asante. Wewe pia mwanamume mzuri sana. Wewe unatabasamu mara chache, lakini kila unapotabasamu wewe mzuri kabisa. Tabasamu yako ni

kama ile ya mtoto".

Ilikuwa mara ya kwanza mtu aliniambia maneno kama yale.

## 6

Jumatatu ijayo, baraza litakuwa la muhimu sana kwa sababu mashahidi watakuwa wengi, yaani yule mwanapolisi aliyeendesha upelelezi wa muhimu zaidi na daktari wa kisheria aliyefanya upasuaji wa maiti na hasa yule mwenyeji wa kilabu cha Maracaibo. Yule aliyesema amemwona Abdou huku akipita mbele kidogo mtoto alipotoweka. Kwa kweli baraza lile litakuwa la muhimu sana, au tuseme, la kukata maneno, na kwa sababu hii nilitumia siku ya Jumamosi na asubuhi ya Jumapili kwa kusoma hati za kupekua na vitabu vya udaktari wa kisheria.

Jumamosi asubuhi nilienda pia dukani pa karatasi na daftari palipokuwa karibu nyumbani pangu. Kule dukani ilikuwa inawezekana kupata nakala zenye rangirangi. Mwenyeji wa kike wa duka lile alikuwa amenitazama kwa mshangao nilipomwambia nilihitaji nini.

Nilipotoka nje ya dukani, nilifurahi sana kwa kazi yule bibi aliyoifanya na tena kwa vitu nilivyokuwa navyo. Nilifikiri kwamba sasa nilikuwa na uwezo wa kufanya kitu fulani.

Margherita alikuwa amekuja ofisini mwangu siku ya Ijumaa, baada ya mchana. Alikuwa amesoma zile karatasi akitumia zaidi ya saa tatu, yeye pekee yake sebuleni. alimwomba Maria Teresa – aliyekuwa na shaka – ampatie nakala fulani, kisha karibu na saa tatu usiku alipita kuniaga. Kwa wikiendi ataenda nje.

Pamoja na nani? Nilijiuliza kwa sekunde moja tu.

Tutaonana Jumatatu ijayo asubuhi, saa tatu na nusu hivi, kortini. Busu, alisema huku akiondoka. Busu, ningelitaka kumjibu. Bali, nilimwaga kwa konyezo la mkono tu, kisha nilisimama kumtazama, nikifunga mkono pole pole alipotoka chumbani.

Kwa bahati nzuri, wakati wa wikiendi ile hali ya hewa ilikuwa bado ya baridi kidogo, kwa hiyo, niliweza kufanya kazi bila kupata matatizo



mengi.

Siku ya Jumapili, karibu na saa saba na nusu mchana, niliona nimechoka kabisa na niliamua kutoka nje. Saa ile niliweza kwenda baharini tu. Mjini na njiani pasipo na watu kwa hiyo nitafika po pote nitakapo. Nilichukua mzigo, nilitia taulo ndani yake na vazi la kuogelea, kitabu kimoja na, baadaye, nilitoka nje.

Kwa kweli mjini pasipo na watu na nilipapitia nikitumia dakika chache tu kuelekea pwani, nikiacha nyuma yangu hoteli ya zamani iliyoitwa Hoteli ya Mataifa. Niliendesha benzi yangu kwa uvumu wa kupumzisha na, punde si punde, nilifika barabarani. Wakati nilipotaka kutoka nje, nilifikirinitaenda sio mbali sana, tuseme kilometa ishirini kutoka mji wa Bari kama kijiji cha Cozze au cha Polignano. Lakini njiani nilibadili fikra na nilielekea haraka haraka mpaka Capitolo.

Mahali pale pasipojaa watu kama nilivyofikiri na nilishinda kupata nafasi kwa gari karibu na hamamu ambayo – kama nilitambua huku nikishuka garini – ilikuwa kilometa moja tu mbali na mahali ambapo mtoto alitoweka.

Nililipa tiketi kwa gari na kwa kuingia katika hamamu na nilishika njia ya kwenda pwani baada ya kuvua viatu vyangu. Nilijisikia kama sio ya kawaida. Mwaka mmoja ulikwishapita tangu wakati wa hari nilipofikiri ninaenda wazimu. Mwaka uliopita nilichukia nuru ya jua, na pwani, na watu walionekana kuwa hiari yao bali mimi nilichugachuga popote.

Siku hizi nilijisikia kama nimepata ashekali. Nilikuwa nikiangalia watu, na bahari na pwani niliyoichukia mwaka jana na nimeshangaa kwa sababu sikuuma kabisa nikitazama vitu hivi vyote. Nilikuwa nikisihi kama ubaridi mtamu na nimepata tatizo fulani nikifikiri kwamba kabla ya mwaka jana, nilikuwa vibaya hivi.

Ule niliosihi ulikuwa mshtuko usio wa kawaida yaani wenye huzuni kidogo, mzuri lakini.

Nilivua mavazi katika kijumba, nilipangisha kiti cha kutandamia na nilikiweka karibu sana na pwani. Bahari ilikuwa kama navyoipenda mimi, yaani tulivu lakini yenye mawimbi madogo na upepo uliokunja maji. Jua lilikuwa kali lakini sio sana yaani joto la kufumbisha macho na kulalisha pamoja na kitabu mchangani karibu na kiti. Na mi nilifanya hivyo na sauti za watu waliokaa pwani ambazo zilitoweka katika hali njema niliyokuwa nayo.

Niliota ndoto kama inavyotokea kila unapokuwa katika hali iliyo kati

ya kesha na usingizi au, kadhalika, kati ya usingizi na kesha.

Ndotoni mi nakutana na Sara njiani, karibu na nyumba yetu, ninamaana karibu na ile iliyokuwa nyumba yetu na siku hizi ilikuwa nyumba yake tu. Yeye ananilaki, ananikumbatia na kunibusu mdomoni. Mimi pia ninamkumbatia lakini najisikia kama mwenye mgogoro. Kwa kweli – ndotoni – miaka minne imeshapita tangu mara ya mwisho tulipoonana nakuwasiliana. Ninamwambia. Yeye ananitazama akiniuliza kama mi mwendawazimu, lakini uso wake ulikuwa ule wa mtu anayeogopa na karibu kulia. Ninamwambia tena kwamba miaka minne imeshapita na ndio wakati ule anaanza kulia kama mwenye kukata tamaa.

Nasikitika hali nikifikiri kwamba ile ni ndoto tu na nataka kufumbua macho. Lakini kwa muda mrefu nilishindwa kuamka nikibaki katika ile hali iliyokuwa kati ya kesha na usingizi pamoja na sauti za watu waliokuwa pwani.

Halafu nilisikia minyunyo ya maji usoni pangu na kifuani, na sauti niliyoitambua mara moja. Sauti ya Elena.

"Guido! Guido, tangu zamani!".

"Elena, nafurahi…".

Mwongo, mwongo kabisa, nilifikiri. Mimi nilikuwa nimemchukia Elena tangu zamani. Yeye na mume wake mbaya na wale marafiki wake wabaya. Alikuwa amesoma pamoja na Sara katika Shule ya Sekondari na Chuo Kikuu na alisadiki sana kwamba alikuwa dada yake wa moyo. Sara alifikiri kinyume lakini hakupenda kuwa mtovu wa makini naye. Kwa hiyo tulilazimishwa, muda kwa muda, kwenda kula pamoja na Elena na, mara kwa mara, kumkaribisha kwetu pia.

Alipoinama ili anikumbatie niliona amenukia herufu kali ya *Opium*. Ametumia manukato ya *Opium* baharini? Nilikuwa na hakika kwamba, mimi na Sara tulipoachana, yeye alikuwa amesema mengi juu yangu, na maneno yake yalikuwa ya kusikitisha. Na sasa, kulingana na tabia yake, alikuwa akinikumbatia na kunibusu hali akiniuliza nilifanya nini wakati ule.

"Guido, naona hali yako nzuri kabisa! Umefanya mazoezi ya mwili kipupwe kilichopita? Wewe peke yakoau una mchumba fulani?". Alionekana kama akisema: "*niambie tafadhali, mimi nitaandika tangazo kwenye gazeti fulani na mabango mamia tena mjini*".

"Ndio, mwanaharamu we', mimi peke yangu na ningependa kuendelea kuwa vile vile. Walakini, kwa kuwa umefika hapa kunichosha, nina ya



kukuambia, kwa hiyo sikiliza kwa makini. Chakula chako kilikuwa cha kutapisha tu na kila tulipokuwa pamoja, sisi tulichoka kama nini. Najua kwamba wote walisema wewe mpishi mkubwa lakini habari hii kwa maoni yangu ni fumbo, na itaendelea kuwa hata milele. Na, ikiwezekana, mumeo ni mbaya zaidi. Na marafiki wenu, ikiwezekana, wabaya kabisa, zaidi kuliko yeye. Mara moja wamenitia moyoni nijiandike Rotary Club. Nataka kukuambia mimi *mkomunisti*. Wakati wa tafrija nyingi za jioni na tena kwa miaka mingi umekula pamoja na *mkomunisti*. Umeelewa? "

Maneno haya na tena mengine ningalipenda kuyamwambia. Lakini nilimjibu kwa adabu. Ndio, nilikuwa mi peke yangu, hapana, sikuwa na mchumba, ndio nasema kweli, hapana, sijamwona Sara tangu zamani. Ah, yeye pia alikuwa hapa baharini na tena peke yake? Alikuwa amepata taabu kwa Mario? Kwa kweli, ni rahisi sana kupata matatizo kwa Mario. Na kwa Sara pia, bila shaka. Tuonane wote pamoja jioni fulani? Yeye na mimi? Ndio, hamna shida. Namba yake ya simu ninayo? Nafikiri ninayo. Ah, haiwezekani kwa sababu alikuwa na namba mpya. Sawa, kwa hiyo lazima aniipatie. Na mimi, nitampigia simu? Anatumaini. Ndio, asiwe na wasiwasi. Ndiyo. Kwa heri. Tuonane mapema. Busu, *Opium*, busu nyingine na ukonyezo wa jicho mwishoni.

Nilizama nione maji yalivyo na nifute *Opium* toka ngozini. Maji yalikuwa ya baridi sana. Iwayo yote ulikuwa bado mwezi wa sita na hali ya hewa ilikuwa baridi kwa kawaida. Niliogelea kidogo kwa sababu, nilifikiri, lile lilikuwa chovyo langu la kwanza na niliamua kwenda kutembelea pwani.

Wachezaji wa tufe nyororo na vibao walikuwa wachacheyaani sio wengi kwama walivyo wakati wa mwezi wa saba au wa nane. Ningalipenda kuwaua lakini, kwa sababu zile zilikuwa siku za kwanza za kiangazi, ningewapatia kifo cha ghafula. Mwezi wa saba au wa nane ningalipenda kuwaua kwa maumivu makali. Mi ninawachukia sana wachezaji wa tufe nyororo na vibao, lakini hali nilikuwa nikitembea – nikijitahidi kuwachokoza nikitembea kati ya njia ya mipira itupwayo ipitavyo hewani – nilimwona binadamu ambaye namchukia zaidi kuliko wale wachezaji. Yaani, mvutaji wa kiko pwani.

Mimi siwapendi wavutaji wa kiko. Nachelea kila ninapomwona mtu fulani anayevuta kiko njiani. Lakini nachelea sana nikimwona mtu fulani – kama ilivyokuwa siku ile – anayevuta kiko pwani hali akipesapesa kwa kiburi kama Sherlock Holmes. Akivaa chupi tu.

Nilikuwa nimewafikiria wavutaji wa kiko na wachezaji na niliona kwamba nilikuwa nimepata sijambo nikijirudishia ushupavu wangu wa zamani.

Wakati ule ule nilimwona kijana mmoja mweusi aliyebeba bidhaa za aina mbalimbali, zilizotundikwa kwa fimbo begani pake na katika mzigo uliofumuliwa na kufunguliwa nusu. Alivaa kanzu yenye rangirangi na ndefu na kofia kichwani. Nilisimama nikikaa kwa miguu baharini. Nilimwangalia kwa muda kabla nitambwe kwa sababu gani nilikuwa nikimwangalia hivyo.

Nilipotambua na bila maana niliamua itakuwa vizuri kumwangalia huku alikuwa akifanya kazi yake pwani. Ni wazi kwamba sikuwa na fikra fulani kuhusu yeye. Mara fikra ya kumwuliza akimjua Abdou ilinijia akilini. Lakini niliiacha na nilimwangalia tu.

Alionekana amezoea kupita kati ya viti vya kutandama na vitambaa vikubwa vilivyokuwa vimewekwa pwani. Kwa utaratibu aliwasalimu kwa mkono mabibi waliokuwapo, na wale walimsalimu. Mmoja wao alimwita kwa jina ambalo sijalielewa. Yeye aligeuka na alimwendea akitabasamu, aliweka vitu vyake chini, alimpa mkono na, baadaye, alianza kuzungumza. Ni wazi kwamba alikuwa akionyesha bidhaa zake. Alisimama zaidi ya dakika tano na mwishoni, yule bibi alinunua mkoba mmoja. Yeye alianza tena kutembea na mimi niliendelea kumfuata. Mwanzoni kwa macho tu na baadaye kwa miguu, nilimfuata nikibaki mbali naye kama mita ishirini hivi. Onyesho nililoliona lilirudisha mara nyingi kwanusu saa. Na bila sababu niliamua kumpitia karibu, ili nimwangalie tu na kuondoka baadaye, kwa sababu kumwangalia tu kumenichosha. Nilipokuwa karibu sana naye, yaani nilikuwa nikitembea kando yake kadiri ya kumpapasa, nilisikia mlio mkali uliotoka mzigo wake. Alisimama na alichukua simu ya mkononi aina ya ‚Motorola', tena ya zamani.

Alisema *Alo* kama Wanegro katika filamu hafifu, yaani *Alù*. Ndio hivyo. Nilifikiri kwamba akiwa Mchina atasema *Lo*. Kwa kweli, fikra hii ilikuwa ya kipumbavu. Lakini ilikuwa fikra iliyonijia akilini wakati ule.

Mazungumzo yalikuwa ya kifupi na kwa kiitaliani. Yaani kwa aina ya kiitaliani.

Ndio, alikuwa akifanya kazi. Pwani, rafiki yangu. Ndio, kuna watu wa kutosha. Ndio, rafiki, Monopoli, pwani ya Capitolo. Ataweza kuja kesho, kesho asubuhi. Sawa rafiki, kwa heri.

Alifunga simu ya mkononi na alianza tena kutembea. Mi nilisimama,



kwenye pwani nilipopiga magoti ili nisikilize simu ile. Nilikuwa jambo lililonijia akilini.

Na nilijiuliza kwa sababu gani bado sijalifikiria.

## 7

"Wajua, Guido, umri wetu ni umri mzuri zaidi. Tunaweza kufanya kila tunachotaka".

"Vipi' Una maana gani?"

"Kumbe, wewe ndiwe, Guido. Tangu ukae peke yako, bila shaka, hufanya mapenzi ovyo, bila matatizo. Kumbe, na unaniuliza pia mi nina maana gani?".

"Ah, nafanya mapenzi ovyo", nilisema kwa sauti isiyoonyesha furaha.

"Hebu, Guido, una nini? Tumekutana tangu mwaka jana, labda zaidi, na sasa hunisimulii kitu?"

Nilikuwa nikitembea kwa haraka kidogo kuelekea baraza ya hukumu, nikishika mizigo miwili mizito iliyokuwa na ndani yao maandiko niliyoyahitaji kwa barazani. Rafiki yangu, jina lake Alberto, alinifuata akijitahidi kidogo kwa sababu ya unene na kukaakaa. Tulikuwa tumekutana njiani na mwaka mmoja ulipita tangu tulipoonana kwa mara ya mwisho. Yeye alikuwa na miaka arobaini, na watoto wawili na mke mnene na mwovu.

Alikuwa ameirithi ofisi kwa babake na alikuwa akishughulikia mambo ya benki na ya bima, kwa hiyo amepata faida sana. Hoja aliyoipendelea ndio 'mapenzi'. Kwa kweli alikuwa mtaalamu lakini kwa maneno tu.

Alipokuwa kijana mpendevu, mwenye tabia ya mzaha. Huzoea kusema matusi na kwa jinsi alivyoyasema alituchekesha sisi marafiki sote. Angalifanya kazi nyingine labda atakuwa mchangamfu. Bali alichagua kufanya kazi kama mwanasheria. Miaka ilipita na ucheshi wake pia ulimalizika kuwa pamoja na nywele zake na zote za thamani. Alberto aliendelea kusema matusi lakini – nilifikiri asubuhi ile – hakuchekesha tangu zamani. Alikuwa mtu mwenye kukata tamaa lakini bado alikuwa hajajua.

"Sina ya kusimulia, Alberto, ni kweli. Mi uhusiano wa kipenzi sinao".

"Eh! Wasemaje? Na sasa hivi unakaa wewe peke yako, waweza kufanya yote utakayo".

"Ndio. Maisha ni ya ajabu, si ndio?"

"Ah, si umekuwa msenge?". Na aliendelea kwa hadithi juu ya mtu fulani ambaye ingenipasa kumjua au kumkumbukia. Sijamkumbuka lakini sijamwambia Alberto. Huyu mtu – jina lake Marco – alioa na alipata pia mtoto mmoja. Baada ya muda mfupi, mkewe alitahamaki mambo yasiyo ya kawaida, akasadiki kwamba mumewe ana hawara. Kama wanavyosema, alikuwa amemwajiri *mpelelezi* aliyefanya kazi yake vizuri sana. Alichunguza uzinzi. Lakini kumbe! Marco hakuwa na mchumba wa kike bali *wa kiume* aliyefanya kazi ya mchinja wanyama.

"Loh! Umeelewa Guido? Mkewe alifikiri yeye mpenzi mkubwa aliyezoea kufanya mapenzi na visichana na, kinyume chake, huyu ni mfiraji ambaye hufirwa na mchinja wanyama. Haki ya Mungu! Mchinja wanyama. Labda humpatia soseji za nyama ya farasi kwa chakula cha saa kumi... Si umefuata wewe pia mwenendo wa ufiraji na hufirwa na, tuseme, mwuza nyama ya nguruwe?".

Hapana bado sijafuata mwenendo wa ufiraji – nilimtia moyo – na nimejitahidi kutofiriwa na yeyote.

Tulifika mlangoni pa baraza ya hukumu na wadi yetu ya kuagana na kwenda kazini imetimia. Lazima tukutane tena pamoja na marafiki wengine. Alitaja majina fulani niliyosikia kama kumbukumbu tu. Tungeweza kula piza au kucheza mchezo wa karata. Haya, bila shaka utakuwa mkutano mzuri sana. Ndio, ndio tuwasiliane wiki hii au ile ijayo. Kwa heri Guido – kumbe – nimefurahi kuonana nawe. Kwa heri Alberto. Mimi pia.

Alielekea lifti ya kuenda orofa ya tano, yaani mahali pa daawa tu. Mi nilisimama kumtazama nikifikiri kwamba zamani na katika mahali pa mbali tulikuwa marafiki.

Nimefikiri haya kama mtu ashukuye.

Kumenijia kusema 'Alamsiki, Alberto' na nilimwaga kwa sauti ya chini iliyosikika na mtu fulani akiwapo karibu nami.

Lakini hakuna mtu.

Kabla kesi isikilizwe mi nimewahi kuzungumza na Abdou. Nilikuwa na nia ya kuhakikisha kama fikra zilizonijia kule pwani zilikuwa na maana kwa kuziendeleza.



Ilikuwa yamkini. Labda tulikuwa tumepata fursa zaidi lakini nimejaribu kuzuia harara zozote. Sababu ni kwamba, kwa desturi, inapokujia fikra inayoonekana kuwa nzuri kabisa baadaye ndiyo fikra hii haifai na wewe utasikitika tu.

Nilikwisha ona kwa majaribio mara nyingi lakini sio ya kutosha ili niache.

Margherita alifika saa tatu na nusu barabara. Alinisalimu kwa tabasamu toka kwa mahali pa kukaa pa watazamaji. Nilimwashiria aje karibu nami. Hakukubali kwa kichwa na kwa mikono alinikonyezea akakaa vizuri kule alikokuwa. Nilimkaribia mimi.

"Joho linakupendekeza" aliniambia.

"Asante, njoo na keti karibu nami. Umeshashinda mitihani kwa kuwa mwanasheria. Unaweza".

Alicheka kidogo.

"Kama nijuavyo mimi, nimeshaandikiwa kwa Chama cha Wanasheria. Babangu hakukata tamaa na aliendelea kunilipia kodi. Nikitaka, naweza kuanza kufanya kazi kama wakili wakati wowote".

"Sawa kabisa. Basi, njoo na keti karibu nami. Ukipenda kuona mashtaka yataendeleaje, kile ndicho kikao cha kufaa kabisa".

Alikubali kwa kichwa na kuja nami. Aliketi upande wangu wa kulia. Nilipenda sana awe kule, amenitia moyo".

Tulianza maulizo kwa daktari ya kisheria aliyefanya uchunguzi wa maiti. Huyu alithibitisha yote aliyoyaandika kwenye ripoti ya uchunguzi wa maiti. Alisema kwamba mtoto alifariki kwa songo wa roho. Alisema pia kwamba hakuweza kuwapatia mahakimu habari nyingine yaani sababu za msongo wa roho, ndio nyingi. Mtoto alikuwa amenyongwa tu kwa sababu hazikuwapo alama za mivunjo. Labda mwuaji alimzuia mtoto pumzi kwa mto akimfunga mdomo na pua na halafu akamficha kwenye nafasi ndogo sana kama, kwa mfano, ile ilitumiwa garini kwa kubebea mizigo. Ilikuwa inawezekana pia – na katika vitabu vya maarifa yaliandikwa mengi kuhusu kesi za jinai sawasawa – kwamba msongo wa pumzi ungalisababishwa na tendo la kufanya mapenzi kwa kunyonya sehemu za siri za kiume na tena kwa ukali.

Kwa kila hali hazikuwapo alama za ubakaji wala za shahawa. Mtoto alipokutwa amevaa mavazi yale yale yaliyovaliwa naye siku alipotoweka.

Alipotumbukizwa shimoni, mtoto alikuwa ameshakufa kwa sababu mapafuni hamna maji.

Mi sikuwa na nia ya kumwuliza swali daktari. Niliomba aeleze vizuri zaidi kwamba marejeo kuhusu kufanya mapenzi kwa kunyonya sehemu za siri za kiume na kwa ukatili zilikuwa fikra zake daktari na kwamba hazikuwapo alama za kweli kuhusu ubakaji wa aina yoyote.

Daktari alipomaliza kusema, Mwendesha mashtaka alimwita afisa wa kiaskari, jina lake Lorusso, ili atoe ushuhuda wake. Huyu alitawala askari wa mjini Monopoli na yeye alikuwa shahidi wa muhimu zaidi kuliko ya wapelelezi wengine. Yaani, kwa upelelezi ule, yale matendo machache ya maana yalitendwa naye. Mimi nilijuana naye tangu zamani. Nilikuwa nimeshakutana naye kwa mashtaka mengine na nilijua kwamba alikuwa mtu asiye wa kawaida. Ukimwona, utaweza kufikiri kwamba anafanya kazi kama karani au mwalimu. Ni mtu mwenye nywele chache za rangi ya kimanjano, alivaa miwani midogo, koti na tai vinavyouzwa sokoni. Mara mzee Lorusso alionekana kama mwenye tabia isiyodhuru. Lakini ukiweza kuyatazama macho yake nyuma ya miwani, utayatambua kama macho yake mtu mwenye akili nyingi. Zamani alifanya kazi katika sehemu ya kijinai ya polisi mjini Bari, halafu alifatiwa pamoja na kepteni na mwanapolisi mmoja katika kesi ya jeuri juu ya mtu aliyekamatwa nao. Wote walihamishwa na Lorusso akalazimishwa kuwazoea kuruta shuleni kwa muda wa miaka miwili. Kwa afisa wa kiaskari kama alivyokuwa yeye, adhabu ile ilikuwa kali, kwa kweli.

Maulizo yaliyoendeshwa na Cervellati yalidumu zaidi ya saa moja. Shahidi alihadithia kuhusu jinsi ya kutafuta mtoto na jinsi walivyowakuta mashahidi, akaendelea kuongea kuhusu kukamata kwa Abdou na upekuzi.

Alisema kwa mng'ao wa maneno. Mzee Lorusso ni mtu asiyedanganyika.

Kama ya kawaida, wakili wa jamii hakuwa na swali na hukubaliana na mambo yaliyofanywa na Mwendesha mashtaka.

Baadaye, Mwenyekiti wa Mahakimu aliniruhusu kusema.

"Shikamoo, mzee".

"Marahaba". Alijibu bila kuniangalia. Kwa kweli akiwa na akili nyingi ameelewa kwamba nilikuwa nimekunjukiwa ili niwatekeze wale mahakimu wa jamii kwa usemi wangu.

'Acha kupayapaya, wakili we' na onyesha unataka nini', Alikuwa amezificha fikra hizi kwa salamu yake. 'Sawa', nilifikiri mimi binafsi.

"Tafadhali, sema tena, unafanya kazi gani?".

"Ninatawala kundi la kiopereta la kombania ya mji wa Monopoli".



"Na, kabla ya kazi hii, ulipatiwa tume gani?" Afadhali twanze kucheza mchezo bila huruma sasa hivi, nilifikiri.

"Lakini mambo haya hayafai", nilipata shabaha.

"Tafadhali, unaweza kutuambia ulipatiwa tume gani kabla ya kazi hii?"

Alisisitiza kidogo, alionekana alitaka kumwangalia Mwendesha mashtaka na akikunja uso wake alijibu.

"Nilifanya kazi kama mwalimu kwa kombania ya kuruta mjini Reggio Calabria".

"Kama nimeelewa vizuri, kazi ile haikuwa kazi kwa polisi ya kihukumu".

"Ndio".

"Na mwanzoni kabisa?".

Sasa Cervellati alijiingiza.

"Samahani, Mheshimiwa. Lakini sioni kama mambo haya ni ya muhimu kuhusu maulizo hayo".

Mwenyekiti wa Mahakimu alinigeukia.

"Kwa nini umetoa maswali yanayohusiana na kazi za kwanza za shahidi?".

"Mheshimiwa, lazima nitoe maswali haya mbele ya sheria zinazoainisha makosa na adhabu zake, yaani ibara yenye namba 194, kipande cha pili cha mwandiko. Na kama utakavyoweza elewa baadaye, majibu ya shahidi yatanisaidia ili niweze kutia maanani maneno ya mzee Lorusso".

Mwenyekiti wa Mahakimu alibaki kimyani wakati hakimu wake akamnong'oneza maneno fulani sikioni mwake. Mwishoni, baada ya kimya kidogo Mwenyekiti wa Mahakimu aliniashiria kwa konyezo la mkono niendelee.

"Basi, mzee, ulifanya kazi gani kabla ya kuwafundisha kuruta?".

Wakati nilikuwa nikitoa swali hilo, mzee lorusso alinitazama kwa chuki. Nilitaka kutenda tendo lisiloruhusiwa yaani nilitaka kuvunja mkataba wa kutoshambuliana uliyoko kati ya wanasheria na wanapolisi wakati wa mashtaka. Yeye alielewa. Akiwa n anafasi atajilipiza kisasi. Nina hakika.

"Nilikuwa nifanya kazi kwa jamii ya mapolisi, kikosi cha kiopereta mjini Bari, sehemu ya kwanza, katika Idara ya upelelezi wa Jinai".

"Yaani kikundi kinacho wapelelezi watangulifu wa mkoani. Kwa hivyo, kama nimeelewa vizuri, wewe ulikuwa umepitishiwa kazi kama mpelelezi

mtangulifu kwa kazi ...tuseme, kama mwalimu kwa kuruta mjini Reggio Calabria. Sawa?".

"Ndio".

"Lilikuwa fuatano la taratibu au lilitokea kwa sababu nyingine?".

Kwa kweli, nilikuwa sijapenda yale niliyotaka kuyafanya lakini lazima nimkasirishe kwa kupitia yale niliyotaka kwa kweli.

"Samahani, lakini wewe wajua kwa sababu gani wamenibadilisha kazi na tena wajua kwamba tangu hapo naweza kupiga pua".

"Unaweza kutuambia unazungumzia historia gani?". Sauti yangu ilikuwa ya moyo lakini, kwa kweli, yenye uwongo. Tuseme, nilikuwa mtu wa kuchukia.

Mwenyekiti wa Mahakimu alijiingiza n amara hii bila kumsubiri Mwendesha mashtaka.

"Wakili, angalia usitumie vibaya ustahimili wa jamii ya mahakimu. Nena kweli".

"Mzee, naomba tuambie kwa sababu gani ulihamishiwa mjini Reggio Calabria?"-

"Kwa sababu jangiri aliyekamatwa katika kuuza kilo moja ya kokeini na mwenye kurasa tatu za cheti cha adhabu, alikuwa ameshtaki mimi na kepteni na mwanapolisi mwingine akisema tulikuwa tumempiga. Wote watatu tuliondolewa hatia na yule bwana alihukumiwa miaka kumi kwa kuuza madawa ya kulevya, Inatosha?".

"Wewe umesikia maneno ya bwana Renna yaani mwenyeji wa kilabu kinachoitwa 'Maracaibo', na yale ya Wasenegali wawili yaani bwana Diouf na... sasa sikumbuki jina la mtu mwingine. Kulahali, ni sawa?"

"Ndio".

"Naomba uwaambie jamii ya mahakimu kama ulivyoandika kitenzi cha tendo?"

"Una maana gani?".

"Mmerekodi sauti kwenye kinasasauti au mmepiga picha za video?".

"Hatukurekodi maneno. Ukisoma vizuri vile vitenzi vya matendo, utajua kwamba tuliandika muhtasari wa matangazo yao kwa sababu rekodi tuliyokuwa nayo haikufaa".

"Ah, ndiyo. Haya, kama nimeelewa vizuri, nyinyi mmeandika muhtasari kwenye kitenzi cha tendo kwa sababu rekodi na kurekodi cha mkanda wa video havikufaa. Sawa?".

Mzee Lorusso alielewa fikra zangu, lakini amechelewa mno.



"Kwa muda ule sidhani... tulikuwa tukifanya kazi katika dharura..."

"Lazima nikuulize swali rahisi sana: kwenye kituo cha polisi mjini Monopoli, nyinyi hamkuwa na rekodi au kamera ya video?".

"Tulikuwa navyo, lakini wakati ule... nadhani rekodi haikufaa. Sasa sikumbuki lakini, bila shaka, tulishindwa kusawazisha tatizo lile".

"Basi, rekodi haikufaa, na kamera ya video?".

"Hatunayo".

"Samahani, mimi nina hapo mbele yangu kile kitenzi cha tendo chenye habari za kukagua mahali ilipokutwa maiti ya mtoto na naweza kusoma kwamba *matendo yote ya ukaguzi yalishuhudiwa kwa kamera ya video*. Na, kwa kweli, pamoja na kitenzi cha tendo uko pia mkanda wa video. Wasemaje?"

Cervellati alijipinga akipiga kelele. Alitaka kukasirika.

"Hapana, Mheshimiwa, hapana. Hatuwezi kusadikika maulizo yanayohusiana na jinsi ya kuandika kitenzi cha tendo, au kama shahidi alitumia rekodi au kalamu au kompyuta".

"Mheshimiwa, kama haisadikiki ni maoni yake Mwendesha mashtaka tu. Mi najali nielewe kama yalivyokuwa yameandikwa matangazo yale ili nihakikishe ikiwa, na hata bila makusudi, kwa sababu hakuna mtu anayeshuku unyofu wa mashahidi, nina maana ili tuhakikishe kama mashahidi walitiwa masharti au maneno yao mashahidi yalikosewa kufahamu. Lazima kutosahau kwamba Mwendesha mashtaka aliomba yasomwe matangazo yaliyotolewa na wale Wasenegali wawili wakati wa upelelezi...".

Zavoianni alinidakiza. Alikuwa akikasirika. Hajapenda yale majadiliano yote, hajapenda jinsi yangu ya kufanya kazi yangu na – nimeshatia shaka tangu zamani lakini sasa nina hakika – hajanipenda mimi.

"Tuendelee kwa mengine. Nimeshajibu maswali mengi ya bure. Hatimaye, endelea na utoe maswali yanayohusiana na mashtaka haya".

Nilipomwangalia Mwenyekiti wa Mahakimu huku anasema, nilishinda kumwona Lorusso aliyekuwa akivuta pumzi na kushusha kwa nguvu akijiburudisha.

"Mheshimiwa, mi nafikiri ndio muhimu sisi sote tujue kwa nini usikizi wa watu wenye maarifa haukurekodi kabisa, na sasa usikizi huu na hasa ule uliotolewa na wale wabwana wasenegali, sisi hatuwezi kuusikia tena kwa sababu haupatikani".

"Nimeshaamua. Endelea na usijaribu kushindana na maamuzi yangu".

Uso wangu umefinyana kwa dakika moja tu. Baadaye, nilianza tena.

"Asante, Mheshimiwa. Je, mzee, naomba uelezeemambo yanayohusiana na upekuzi katika nyumba yake mshtakiwa".

"Na juu ya yote, una taka kujua nini?".

"Kama mlivyokuwa mmepekua, ikiwa mkivitafutatafuta vitu hususan, ilikuwaje hali ya mahali na kadhalika".

"Sijaelewa vizuri swali lako. Sisi tulikichakura chumba chake thiam tukitafutatafuta popote bila kutazama vitu hususan, tumetazamia kila kitu cha kufaa kwa upelelezi kilichokuwa ndani ya chumba. Halafu, chumbani tulipata ile picha ya mshtakiwa pamoja na mtoto na vitabu vya watoto vilivyokwisha andikwa kwenye kitenzi cha tendo".

"Si mmepata vitu vingine vya kufaa kwa upelelezi?".

"Hapana".

"Kama sivyo, mngalivichukua".

"Kama sivyo, tungalivichukua, bila shaka".

"Mmepata kamera ya 'Polaroid' au kamera ya kawaida?".

"Hapana".

"Sikiliza, sasa ningependa kuzungumza nawe kidodo kuhusu vitabu mlivyopata chumbani mle. Kwenye kumbukumbu la upekuzi na utekaji nyara nasoma kwamba bwana Thiam, chumbani mwake alikuwa na riwaya tatu za *Harry Potter*, na riwaya moja inayoitwa *The Little Prince*, na hadithi za watoto kwa kifaransa, na tena hadithi maarufu ya Pinokio na kitabu kingine kinachoitwa *Dr. Dolittle*, sawa?".

"Ndio".

"Bwana Thiam alikuwa na vitabu hivi tu chumbani mwake?".

"Sasa sikumbuki vizuri, Labda kitu kingine fulani".

"Unaposema *kitu kingine fulani*, una maana ya kitabu kingine?".

"Ndio, nadhani kilikwemo kitabu kingine"-

"Karibu sawa, unaweza kusema vitabu vingapi?".

"Sijui. Vitano, sita, kumi".

"Utashangaa nikikuambia kwamba katika chumba kile vilikwemo zaidi ya vitabu mia?".

"Samahani", Mwendesha mashtaka alisema, "unauliza maoni yake shahidi".

"Nitatoa tena swali yangu, Mheshimiwa. Una hakika, mzee, kwamba vitabu vilikuwa zaidi ya kumi?".



"Labda ishirini, sio mia".

"Unaweza kueleza chumba kile na hasa kama zilikwemo rafu?".

"Sasa, mwaka mmoja umeshapita walakini, chumba kile kilikuwa na kitanda, meza ndogo… ndio, labda rafu moja upande wa kitanda".

"Rafu moja, nyingi au kabati la vitabu?".

"Labda… inawezekana kabati dogo la vitabu".

"Sasa, natambua kwamba sio rahisi baada ya mwaka mmoja lakini ujitahidi ukumbuke kilikuwamo nini katika lile kabati dogo".

"Sikumbuki. Bila shaka vitabu vilikuwapo, lakini sina makumbuko ya vitu vingine".

"Bila shaka umeelewa kwamba nia yangu ni kuonekana, kwa nasibu, vitabu vingapi vilikuwamo – Mi ninavijua, lakini ningependa ungekumbuka wewe mwenyewe".

"Zilikuwamo rafu nyingi na vitabu, lakini siwezi kusema vingapi".

"Lakini nyinyi mmevichukua vichache tu, yaani vile vilivyoandikwa kwenye kumbukumbu la upekuzi tu. Kwa nini?".

"Kwa sababu, bila shaka, vilikuwa vile vya kufaa kwa upelelezi".

"Kwa sababu vilikuwa vya watoto?".

"Ndiyo".

"Nimeelewa. Sasa ningependa kuzungumza kuhusu picha ile ya bwana thiam pamoja na francesco. Unaweza kusema nini kuhusu piche hii?".

"Sielewi swali lako".

"Ile ilikuwa picha ya pekee, bwana Thiam alikuwa nayo au zilikuwapo nyingine?".

"Sikumbuki. Sisi tulikuwa watatu wakati wa upekuzi. Sikumbuki kama picha niliipata mimi au mshiriki wangu".

"Ningependa kukuonyesha kitu fulani". Nilitoa bahasha toka kibogoshi na niliifungua pole pole, nikamwombea Mwenyekiti wa Mahakimu ruhusa ya kuimwonyesha picha shahidi. Mwenyekiti wa Mahakimu alikubali kwa kichwa.

"Unaona picha hizi, bwana? Kwanza, unaweza kusema ukimfafanua mmoja miongoni mwa watu waliopigwa picha?".

Lorusso alitazama picha nilizompatia – labda thelathini – halafu akajibu.

"Kwenye picha nyingi yuko mshtakiwa. Watu wengine mi siwafahamu".

"Unakumbuka au unaweza kukataa kwamba picha hizi zilikuwa

chumbani mwa mshtakiwa wakati wa upekuzi?".

"Sikumbuki na siwezi kukataa".

Umefika muda wa kusimama kwangu nikistahimili kishawishi cha kutoa swali zaidi itakayokuwa ya kupita kiasi.

"Asante, Mheshimiwa, mi nimemaliza maswali. Kama mathibitisho naomba upataji wa picha nilizomwonyesha shahidi".

Nilimwonyesha picha Mwendesha mashtaka wa wakili wa jamii. Hawakukataa ingawa Cervellati aliniangalia kwa chuki. Halafu niliweka tena picha ndani ya bahasha na nikampa Mwenekiti wa Mahakimu.

Lorusso aliondoka baada ya kuwaaga kortini na Mwendesha mashtaka. Alipita mbele yangu akinidharau. Sikuweza kuona kosa lake juu hilo.

Mwenyekiti wa Mahakimu alisema kwamba tulikuwa na kipumziko cha dakika kumi na mara nikatambua Margherita alikuwa amebaki kwa muda wote karibu nami, bila kusema neno.

Nilimkaribisha kunywa kahawa. Alikubali kwa kichwa. Mimi ningependa kumwuliza anafikiri nini. Yaani ikiwa ameniona hodari na mambo kama haya, lakini lilikuwa swali la kitoto – nimefikiri – na sikuitoa. Lakini yeye ndiye alianza kusema wakati tukiingia katika baa iliyokuwa ndani ya Jumba la Mahakama, ambayo ni maarufu kwa kutengeneza kahawa mbaya zaidi mjini.

Ilikuwa ya kuvutia – alisema – ingawa nionekane kama kwamba mi mtu tofauti. Nilikuwa hodari, lakini sikuwa, tuseme, napendeza sana. Je, ilikuwa lazima nimfedheheshe Lorusso hivyo?

Nilitaka kusema kwamba sidhani nimemfedhehesha na kwamba mashtaka kama haya lazima yawe makatili. Na ukatili huu ulikuwa dhamana ambayo hatuwezi kuacha na, walakini, afadhali askari au mwanapolisi wanaovunjiwa heshima kuliko mtu asiyekosa atakayehukumiwa.

Kwa bahati nzuri sikusema neno. Walakini nilibaki kimya kwa muda mfupi kabla ya kujibu. Nilisema sikuwa na hakika kama ilikuwa lazima kufedhehesha. Lakini ilikuwa lazima kuoneka mambo yale yaliyokuwa ya muhimu na labda njia nyingine ilikuwapo labda haikuwapo. Walakini katika hali kama zile, nina maana katika mashtaka, na hasa yale ya muhimu yanayotazamisha vyombo vya habari na kadhalika, ni rahisi uonyeshe ile tabia yako mbaya tu. Ni rahisi pia upendezwe na kuwatesa watu kwa udhuru mara kwa mara kazi yetu ni chafu lakini mmoja lazima



aifanye.

Tulikunywa kahawa na tukaanza kuvuta sigara. Kwa bahati nzuri, tuliacha mazungumzo kuhusu maadili ya wanasheria. Mi nilisema kwamba kahawa iliyouzwa kule ilitumiwa kwa kuwaua panya. Yeye aliangua kicheko na alisema amependa mi ninamchekesha. Mi pia nilifurahi.

Halafu tulielekea tena darasani kwa baraza la Mahakama ya Rufani.

## 8

Hakimu alimwomba afisa wa hukumu aingize shahidi aliyeitwa Antonio Renna.

Alipitia chumba akipesapesa kwa ujasiri mwingi. Sura yake ilikuwa ile ya mkulima. Ni kibarango, alivaa shati lenye michoro ya miraba na ukanda wa shingo mtindo wa Sabini, alikuwa na ngozi yenye rangi ya kahawia na macho yanayolimuka. Lakini ujanja wake ulikuwa sio wa kupendekeza bali wa aina ya *upesi niwezavyo nitakughilibu*. Aliinua surali toka mkumbuu wa kiunoni kwa konyezo nililoona kama la kinyaa, halafu aliketi taratibu mahala pa shahidi alipomwonyesha afisa wa hukumu. Alimpa Abdou kisogo. Alistarehe kitini akijaa kiti kizima na kuegemeza akijiburudisha mgongoni pa kiti. Alionekana mkinaifu nami nilifikiri nataka kumkomesha.

Maulizo aliyotoa Cervellati yalikuwa kama nakili ya yale yaliyotolewa wakati wa upelelezi wa mwanzo. Renna alisema maneno yale yale na karibu katika fuatano lile lile.

Hatimaye, ilipofika zamu yake Cotugno alitoa maswali yasiyo na maana. Alifanya hivi ili awaonyeshe wateja wake, yaani wazazi wa mtoto, kwamba yeye alikuwapo na alikuwa akipambania kipato mshahara wake.

Nilitaka kuanza maulizo Margherita aliponinon'goneza sikioni.

"Sijui kwa nini, lakini huyu anaonekana ni mtu asiye na heshima yo yote".

"Najua", nilimjibu. Halafu nilimgeukia shahidi.

"Shikamoo Bwana Renna".

"Marahaba".

"Mimi naitwa Guerrieri na ninamtetea Bwana Thiam. Sasa nitakuuliza maswali ambayo naomba ujibu kwa kifupi na bila maelezo". Sauti yangu ilikuwa ya kuchukiza kwa makusudi. Nilitamani kumkasirisha ili nione nikishinda kuikuta nafasi ndogo na kumchukiza. Kama kwa upigano wa ngumi.

Bwana Renna aliniangalia kwa macho yake yanayofanana na yale ya nguruwe. Halafu alimgeukia hakimu.

"Mheshimiwa, inanibidi nijibu masuali yatakayotolewa na mwanasheria?".

"Lazima ujibu, bwana Renna". Uso wake hakimu umeonyesha kwamba, akiwa na uwezo, angeepukana nami na wanasheria wengine. Kwa bahati mbaya hakuwa na uwezo huu. Walakini mi nilifaidi kidogo. Msimamizi wa baa alidanganywa na sasa alikuwa mtu anayeweza kujeruhiwa.

"Basi, bwana Renna, wewe umemwambia Mwendesha mashtaka kwamba tarehe tano, mwezi wa nane 1999, alasiri, umemwona bwana Thiam akitangatanga toka kaskazini kwelekea kusini. Sawa?".

"Ndiyo".

"Unakumbuka wakati wa upelelezi umejadili lini na Mwendesha mashtaka?".

"Nafikiri baada ya wiki moja".

"Na umejadiliwa lini na wanapolisi?".

"Kabla, kabla ya siku moja".

"Na watu wa nchi za ng'ambo huzoea baa yako?".

"Sio wengi. Wanakuja, wanakunywa kahawa, wananunua sigara".

"Unaweza kutuambia watu hawa wametoka taifa gani?".

"Sijui. Wote weusi...".

"Na kwa vyo vyote unaweza kutuambia *weusi* wangapi wanazoea baa yako?".

"Sijui. Ndio wao wanaouzauza pwani na barabarani pia. Mara nyingi wanasimama mbele ya baa yangu".

"Ah, wanasimama mbele ya baa yako pia. Na si wanavunja utaratibu wa biashara yako?".

"Wanaudhi, wanaudhi, wanaudhi kweli".

"Basi, lakini kama kweli wanaudhi kwa nini wewe huwaitii askari polisi au wanapolisi?".



"Kwa nini siwaitii? Mi nawaita lakini wewe umewahi kuwaona wamefika hata mara moja?". Sasa alikuwa amekasirika kwa kweli. Huko nyuma Cervellati alielewa nia yangu. Lakini alikawia mno.

"Mheshimiwa, naona kwamba maswali yanayotolewa na mtetezi bado yasiyohusiana na mashtaka haya. Sidhani itakawezekana kuendelea hivyo".

Kabla Zavoianni hajajitia nilitoa mmi maneno yangu.

"Mi nimemaliza haya. Nataka kupitia mengine".

"Angalia Bwana Guerrieri. Angalia sana", hakimu alisema.

"Basi, bwana Renna, nina maswali mengine kwako... ah, ndiyo, ningependa kukuonyesha picha fulani". Toka kibogoshi niliutoa mkusanyo wa picha zenye rangi. Na nilijimudu kusudi kama mtu mwenye mgogoro.

"Mheshimiwa, naomba ruhusa ili nimkaribie shahidi kwa kumwonyesha picha hizo?".

"Picha gani?".

Sasa nilijifanya tayari kuchecheachechea. Ningalikosa neno moja tu ningaliadhibiwa kwa ajili ya nidhamu. Yaani ningalikosa kusema na yote niliyoyafanya mpaka sasa yangalipotelea mbali.

"Mheshimiwa, hizo ndizo picha za watu wa nchi za ng'ambo – hasa Waafrika. Napenda kuhakikisha kama shahidi anamtambua mmoja miongoni mwao". Nilionekana kuwa mtu asiyependelea upande wo wote.

Hakimu alinikonyezea kwa mkono kama kawaida ili niendelee. Nilitumai Cervellati – akiwa na haki – asitake kupata habari zaidi kuhusu watu wale waliopigwa picha. Kwa bahati nzuri hakusema neno. Mi nilimkaribia shahidi nikizishika picha mkononi mwangu.

"Basi, bwana Renna, naomba uzitazame hizo picha kumi". Nilihisi moyo wangu ulivyopenda mbio.

Bwana Renna alizitazama picha. Sasa hakuwa na raha kabisa kama alivyokuwa mwanzoni mwa baraza. Alisogelea pambizo la kiti kama wanasaikolojia wanavyosema ile jinsi ya kusimama ina maana ya "kutoroka".

"Unamtambua mtu fulani katika picha hizo?".

"Sidhani. Wako wengi, wale wanaopitia baa yangu, siwezi kuwakumbuka wote". Nilitwaa tena zile picha na nilirudi mahali pangu kabla ya kuendelea.

"Lakini, na nisahihishe nikikosa, bwana Thiam ulimkumbuka vizuri,

sawa?".

"Ndiyo, yule hupita kila siku".

"Ukimwona, yeye binafsi au katika picha utamtambua, sawa?".

"Ndiyo, ndiyo, ni yule aliye kizimbani". Wakati ule tu alifanya kama angetaka kugeuka. Mimi nilinyamaza kimya kwa muda mfupi sana kabla ya kutanabahi.

"Wajua, bwana Renna, nilikutolea swali ya mwisho kwa sababu kati ya picha nilizokuonyesha, hasa katika mbili zao uko uso wake bwana Thiam, yaani mshtakiwa. Lakini wewe umesema humtambui mtu. Unaelezaje haya?".

Matukio ya aina hii ndiyo ya ajabu mashtakani, na maishani pia. Walakini yanatokea, sio rahisi kusimulia hisia unazoshikwa nazo. Nilihisi kama kwamba wakati umepunguza mwendo na tena hangaiko hewani na juu ya ngozi yangu. Nilihisi macho yake Margherita yaliyonitazama na nilikuwa na hakika kwamba sio lazima nimwulize kama nilikuwa hodari. Mi nilikuwa hodari.

"Nionyeshe zile picha....". Sasa alikuwa amebadili usemi ambao sasa ulikuwa wa kunitania lakini sio kwa upendelevu. Inatokea.

"Usijali kwa picha hizi. Nakuthibitisha kwamba katika picha mbili hizo yuko mshtakiwa kama jamii ya mahakimu watakavyoweza kuhakikisha nitakapozipokeza. Sasa ningependa kujua unaelezaje – ukiweza – umeshindwa kumtambua bwana Thiam".

Bwana Renna alijibu kwa kilugha, amekasirika.

"Unaelezaje na unaelezaje. Wanafanana wote hawa weusi. Nitasemaje, baada ya mwaka mmoja... Nataka kukuona wewe, nataka kukuona...".

*Simama, simama, simama*. Nilijiambia moyoni mwangu wakati nikihisi kwa nguvu msukumo wa kutoa swali nyingine na kushinda kabisa. Au kukosa. *Simama.*

"Asante Mheshimiwa, nimemaliza. Naomba nizitoe picha, na hasa nakala za picha zilizotumiwa wakati wa maulizo. Zile mbili za mshtakiwa zina mwandiko nyuma zao. Zile nyingine ni za watu wasiohusiana na mashtaka na zimetolewa na magazeti mbalimbali".

Cervellati alitaka kutoa tena swali nyingine kama sheria inavyomruhusu. Kutaka kwake kwa kupata faida yote iwezekanavyo kulikuwa na maana ya kwamba alikuwa amechukizwa.

Alimsemesha tena bwana Renna hadithi yake na kumwelezesha wazi kwamba mwaka uliopita alikuwa na kumbuko zuri na kwamba toka hapo



hakuwahi kumwona tena mshtakiwa, wala usoni wala kwenye picha. Alijaribu kukusanya habari, lakini sote wawili tulijua kwamba itakuwa sio rahisi kuwabadilishia fikra mahakimu wa jamii walizozipata asubuhi ile.

## 9

Margherita hakuja baraza la kufuata – tarehe 21 mwezi wa sita – kwa sababu ilimbidi kumaliza kazi yake. Aliniambia atajaribu yupo pale kwa maulizo ya Abdou, yaani wiki ya baadaye.

Asubuhi ile walisikilizwa wazazi wa mtoto na babu na bibi. Mwendesha mashtaka na wakili wa jamii waliwajadili kwa muda mrefu na tena juu ya mambo yasiyo na maana. Wangeweza kuruka hoji.

Mi nilimwuliza babu swali chache tu. Alikuwa na kamera ya 'Polaroid'? Alikuwa nayo na alikumbuka amepiga picha pwani kiangazi kilichopita. Ilikuwa inawezekana – lakini yeye sasa hakumbuki – kwamba mtoto ameichukua moja zao. Walakini sasa hawezi kusema picha nyingine zipo wapi.

Sikuwauliza swali wazazi wake mtoto na nikiwatazama wakati wa maulizo ya Mwendesha mashtaka, niliona aibu kwa kumwuliza maswali Luteni juu ya mfarakano wao.

Wao walikuwa na umri karibu na ule wangu. Baba mtoto alifanya kazi kama injinia na mama mtoto alikuwa profesa wa kwata. Francesco alikuwa mwana wao wa pekee. Wamejibu swali vile vile na walitenda vile vile yaani walionekana kuwa watu wasiotamani kuwa hai, tena watu wasiokasirika. Walikuwa kama ni mazuzu tu.

Abdou alipisha wakati wote wa baraza akibaki kama amebandikwa kizimbani mwenye uso umesetekwa kati ya mikuo akikaza macho juu ya mashahidi wale kama kwamba angependa kuvuta macho yao na kuwaambia kitu fulani.

Lakini wao hawakutazama mtu na mwishoni mwa ushuhuda waliondoka bila kukiangalia kizimba Abdou alimokuwa amefungwa.

Hawakujali kabisa, hata jinai wa kutazamiwa ataadhabiwa.

Mi nilifikiri kwamba tukizaa mtoto Sara aliponitolea shauri yake, sasa

angekuwa na umri wa miaka sita.

Baraza limechelewesha kwa siku ya Jumatatu ya kufuata kwa maulizo ya mshtakiwa na kwa maombi ya nasibu ya hoja za zaidi kabla ya shindano la maneno.

Nilitoka nje ya chumba cha baraza kilichokuwa cha baridi kidogo kwa kiyoyozi na nilishikwa na joto ya kimaji na tena ya kufisha ya mwezi wa sita. Ilikuwa imefika ijapo ilichelewa. Nilifungua tai na kola huku ninashuka katika daraja kubwa la Jumba kubwa la Hukumu.

Nimetembea kuelekea nyumbani na uvumi usio wa kawaida kichwani. Nilishikwa na wasiwasi kwamba ile hofu niliyokuwa nayo mwaka uliopita inarudia tena na nilikumbuka kwamba toka hapo sijatumia lifti.

Fikra zangu zilianza zimechanganywa pamoja na hofu iliyotaka kunijia. Nilijihisi kama katika maonyesho ya filamu za balaa ambayo mhusika mkuu mwenye kukata tamaa anakimbikimbia huku maji yaliyokuwa yakifurika katika njia ya chini yanamfuata.

Kwa jinsi ya ajabu, fikra hii ilinisaidia. Nilijiambia moyoni mwangu kwamba sasa sina tamaa ya kutoroka. Ningesimama, ningetweta na ningeacha nishindwe na msukosuko. Ijapokuwako.

Nilifanya hivyo yaani nilisimama njiani, nilivuta pumzi na nilikaa bila kutoa pumzi kwa sekunde fulani.

Haikutokea kitu na nilipopumua nilihisi nimepona kabisa na mwenye bongo linalofaa vizuri kama kwamba limesafishwa na magaga ya kizee na wingi wa vigeregenja.

Na hapo ndipo nilifikiri afadhali nipitie ofisini kabla ya kuenda nyumbani. Nilikuwa nimeamua kufanya kitu kimoja.

Njiani kwa kuenda ofisini nilianza kupumua nikisukuma hewa chini ya pazia la tumbo langu kama nilivyofanya kabla ya kila upigano wa ngumi, nikijaribu niwe na akili ili nikaze fikira juu la kufanya.

Nilifika mbele ya mlangoni, nilitoa funguo toka mkobani, niliingia na nilizirudisha funguo mahali pao. Nilifunga shati kwa vifungo na nilifundika tai. Halafu, bali ya kuelekea daraja kama nilivyofanya kwa mwaka mmoja, niliita lifti. Huku lifti ilikuwa ikishuka nilihisi mpwitompwito wa moyo na uso wangu ambao sasa ulikuwa na joto nyingi.

Lifti ilipofika nilijiambia lazima nisifikiri wala kusubiri. Nilifungua mlango wa chuma, halafu vilango viwili vya ndani. Niliingia ndani,



nilifunga tena mlango wa chuma na vilango, nilipiga nambari ya ghorofa ya nane huku ninafumba macho.

Nilisikia lifti limeenda juu na nilifikiri haifai nikifumba macho. Basi, niliyafumbua huku ninasikia nimekokota pumzi na kudhoofika.

Lifti ilipofika ghorofa ya nane nilibaki kama mtu aliyesimama tisti. Nilijiambia haina maana ikiwa nimeshindwa kusimama kule kwa sekunde kumi tena, nikiingie hatarini mtu fulani ataita lifti.

Nilihesabu. Elfu na moja. Elfu na mbili, Elfu na tatu. Elfu na nne. Elfu na tano. Elfu na sita. Elfu na saba. Elfu na nane. Elfu na tisa. Nimemaliza kwa elfu na tisa na mkono wangu juu ya kono la kilango kimoja cha ndani. Niliona mnyeo mwilini mwangu mzima hasa juu ya mkono uliokuwa juu ya kono lile.

Nilikuwa nimesimama wadi.

Elfu na kumi.

Pole pole nilikifungua kilango cha kwanza. Halafu nilikifungua kile cha pili. Mwishoni niliufungua mlango wa chuma. Nilibaki ndani ya lifti ile huku ninatazama sakafu yenye bamba za marmar. Nilifikiri lazima nisiweke miguu juu ya mistari kati ya ubamba na mwingine. Lazima niweke mguu mmoja juu ya ubamba mmoja na mguu mwingine juu ya ubamba mwingine. Nilifikiri kwamba fikra zile ziliniandamana tangu zamani – na bila kufahamu – kila nilipotoka nje ya lifti nilipokuwa nimeitumia lifti.

Nilifikiri: potelea mbali.

Na niliweka mguu wa kwanza katikati ya bamba mbili. nilikukusa kabisa mguu wa pili na nilifunga lifti kwa mkazo wa fikra. Mwanzoni vile vilango vya ndani, nilifunga pia mlango wa chuma na kwa utaratibu.

Nilibaki nimeegamia ukutani kwa dakika kumi nikishika mkoba mbele yangu kwa mikono miwili na mara kwa mara nimeusukisha. Niliangaliaangalia huko na huko kwa macho yasiyo wazi kabisa na nadhani, kwa kicheko kisicho dhahiri mdomoni.

Wadi uliopita nilisogea ukutani. Nilikumbuka kwamba nimemkuta yule karani wa hesabu aliyeitwa Mzee Strisciuglio mwaka jana na nilifikiri itakuwa vizuri nimpigie hodi nimsimulie ilitokeaje.

Lakini sikufanya kitu. Niliingia tena ndani ya lifti ambayo haijaitwa na mtu na niliondoka.

Wadi yangu ya kurudi nyumbani imetimia.

# 10

Wakati wa utotoni mwangu, kila nilipoulizwa nitafanya kazi gani nitakapokua hujibu 'sharifu'. Mhusika mpenzi wangu alikuwa yule mchezaji mmarekani, jina lake Gary Cooper alipoonekana kwenye filamu ya *High Noon*. Walipokuwa wakiniambia kwamba nchini Italia hakuna masharifu na, kupita upeo, wapo wanapolisi tu, mimi hujibu papo hapo nitakuwa mwanapolisi-sharifu. Nilikuwa mtoto mwenye tabia lainifu na nilitaka kuwawinda wabaya, kwa vyo vyote.

Baadaye – nilipokuwa na umri wa miaka minane au tisa – niliona mnyakuzi aliyekamatwa njiani. Kwa kweli sijui alikuwa mnyakuzi au mkwapuzi au namna nyingine ya mkosaji. Sasa, makumbuko yangu yasiyo dhahiri na yanageuka wazi kwa shida n amara chache tu.

Nipo pamoja na babangu na tunatembea njiani. Ghafla, tunasikia mshindo wa kelele nyuma yetu n amara kijana mwembamba anakimbia – nadhani – kama radi kwa uapande wetu. Babangu amewahi kunitenda kabla niangushwe na mtu mwingine anayefika upesi kwa mbio. Yule mtu amevaa fulana nzito nyeusi na anapiga kelele huku anakimbia. Anafoka kwa kilugha. Anampigia kelele kijana asimame au atamwua yeye mwenyewe. Kijana hasimami upesi, lakini baada ya mita ishirini anamgonga mzee mmoja. Kijana anaanguka. Mtu mwenye fulana nzito nyeusi ni juu ya kijana na pale pale mwingine anafika. Huyu ni mnene sana na anatangatanga. Mimi napekua na babangu na ninawakaribia. Mtu mwenye fulana nzito nyeusi anampiga kijana ambaye sasa anaonekana kuwa mtoto. Anampiga konde kuchwani na, kila yule maskini anapojaribu kujilinda kwa mikono anapigwa tena na tena. '*Mwanaharamu. Potelea mbali na kuma mamayo. Mbwa we*' " na ngumi nyingine kichwani kwake kijana anayelia '*Basi, basi*'. Yeye pia kwa kilugha. Halafu anaacha kupiga kelele na analia tu.

Mi ninatazama onyesho hili kama mtu aliyefanyiwa hiponozi. Ninakirihi na tena naona aibu kwa yale niliyoyaona. Lakini siwezi kutokodoa macho yangu.

Sasa anafika mwingine, yaani yule mnene aliye na uso wa kutulia na mi natumai atajitia na atamalizisha matukio yale. Anapofika kama mita mitano au sita na kijana ambaye sasa amejikusanyakusanya, anaacha kukimbia. Sasa anamkaribia kijana akitembea na kutweta. Anapokuwa juu



ya kijana yule anapumua kwa nguvu na anampiga mateke kijana tumboni. Teke moja, na kali sana. Kijana anaacha kulia, anafungua mdomo na anabaki hivyo, ameshindwa kupumua. Babangu ambaye amesimama tuli mpaka sasa, anataka kujitia, anasema kitu fulani. Ni mtu wa pekee miongoni mwa waliopo. Yule mwenye fulana nzito nyeusi anamwambia 'shika lako'. 'Sisi wanapolisi', anafoka. Lakini wote wawili wanaacha kumpiga kijana upesi. Yule mnene anamwinua kijana akimshika kwa koti na anampigisha magoti, kwa mikono iliyofungwa kwa pingu nyuma akiendelea kumshika nywele. Hili ni fundisho punjufu zaidi yote yaani mtoto ameshikwa mkononi mwa wanaume wawili.

Babangu ananitenga na onyesho linatoweka.

Toka hapa niliacha kusema 'nataka kuwa sharifu'.

Jambo lile limenijia mara kwa mara miakani. Pengine nilijiambia moyoni mwangu nimechagua kuwa mwanasheria kama jibu kwa kuchukia onyesho lile. Na mara mara nilidhani ilikuwa hivyo, lakini nikiwa mwenye kiburi tu.

Lakini ukweli ulikuwa mwingine. Nilifanya kazi ya mwanasheria kwa bahati tu, kwa sababu sikupata kazi bora zaidi au nimeshindwa kuitafuta. Yote yalikuwa sawasawa.

Nilijiandikisha kwa elimu ya sheria kwa sababu nilidhani nitapata faida, kwa kuwa sikuwa na fikra wazi. Baada ya digrii nilikuwa nimefikiri nitapata faida nikikoma katika ofisi ya sheria, kwa kweli nilikuwa nikingojea kuwa na fikra wazi.

Halafu niliacha kufikiri hivyo, kwa sababu wakati ulikuwa ukipita nami nilikuwa na hofu kwamba kungojea kuwa na fikra wazi kuna maana. Pole pole, hisia zangu na matamanio na tena makumbuko vimeusingizishwa. Mwaka hadi mwaka. Mpaka Sara aliniondosha.

Hapo ndipo sufuria imeondolewa kifuniko na, toka ndani yake vitu vingi vilienda nje, kwa kweli vitu ambavyo sijawaza na nisingetaka kuviona. Nina hakika hamna mtu atakaye kuviona.

"Kila mtu ana kumbukumbu ambayo angesimulia marafiki wake tu. Ana pia mambo moyoni mwake ambayo angefichia marafiki. Atayajisimulia ndani yake tu na kwa siri. Lakini lazima tuseme kwamba kuna mambo ambayo mtu anaogopa kujiambia na kila mtu mwenye neema ana mambo mengi kama haya yaliyowekwa pembeni mwa moyo wake".

Dostojewskij. *Notes from Underground.*

Nafikiri kwamba sio safi wakati ambapo yale mambo uliyoweka pembeni yanatoka nje. Na tena, yote pamoja.

Nilikuwa nikiwaza mambo haya – na mengine – ofisini wakati ninapanga karatasi za kawaida yaani ninahakika siku za kulipa, ninaandika hati za kirahisi na, zaidi ya yote, ninatayarisha orodha za malipo. Nimelazimishwa, kwa kuwa singalitajirika kwa kumlinda Abdou. Ndani ya ofisini hali ya hewa ilikuwa ya baridi kidogo kwa ajili ya kiyoyozo, bali nje hali ya hewa ilikuwa ya joto sana.

Nilimaliza kufanya kila kitu karibu saa moja. Chumba changu kilielekea kaskazini na kilikuwa na dirisha kubwa upande wa kushoto wa deski yangu. Nilitazama nje, nikaangalia mwanga wa jua ulioangaza roshani ya jumba lililokuwa mbele, halafu nikasikilia uvumi wa kiyoyozo na muziki iliyotoka orofa ya chini.

Ufahamu huu ulikuwa sio wa kawaida kwangu, ukanifurahisha. Nilifikiri natamani kuvuta sigara lakini sio kama kawaida yangu. Mara hii nilitaka kufanya kila kitu kwa utaratibu. Nilichukua paketi ya sigara iliyokuwa juu ya deski, nikaishika mkononi kwa muda mfupi. Niliondosha sigara moja nikiitikisa kwa vidole viwili upande wa pili wa paketi na niliitoa kwa mdomo moja kwa moja. Nilifikiria mara yote nilipotenda matendo yale kama mtu afanyaye mambo yake bila kufikiri wala kutumia akili. Nilifikiri kwamba sasa naweza kufikiria utupu nisizuliwe kwa kichwa, Sasa naweza kukaza macho. Nilihisi kama mwili wanitapa na wakati ule ule tukio moja la huzuni. Niliona kama picha ya meli inayotoka bandarini kwa safari ndefu. Niliwasha sigara kwa kibiriti, nikasikia mpambano wa moshi mapafuni na, wakati ule ule, makumbuko mengi na mengine yalinijia. Lakini sasa siogopi. Ningeweza kusimulia kwa bidii yote niliyoyafikiri huku navuta sigara ile.

Nilipoponda kipande cha sigara katika kikombe cha kioo nilichokitumia kama chombo cha kuwekea majivu ya sigara nilifikiri kwamba mashtaka yatakapomaliza, mi nitakuwa na la kufanya.

Na jambo lile lilikuwa la muhimu sana.



# 11

Ilikuwa siku ya Ijumaa, wakati wa asubuhi, na baada ya kupitia barazani kwa baraza moja la kuanzisha nilienda kumtembelea Abdou gerezani. Maulizo kwake yatakuwa Jumatatu ya kufuata na lazima tujiweke tayari.

Mlinzi ameniingiza ndani ya majilisini na akicheka kidharau alifunga mlango. Ilikuwa joto sana, zaidi kuliko niweze kukisi. Nilivua koti, nilifungua tai na vifunguo vya ukosi wa shati na mwishoni niliamua kwamba sikuwa mfungwa, kwamba sijalazimishwa nikae hapa nikitwetatweta, kwa hiyo nilifungua mlango. Afisa aliyekuwa ushorobani alinitazama kwa ukatili, alionekana alitaka kusema kitu lakini, baadaye, aliacha.

Niliegamia mhimili uliokuwa kati ya chumba na ushoroba. Nilitoa sigara moja lakini sikuiwasha. Joto kali sana kwa kuvuta sigara.

Nilihisi shati langu lililobandikwa mgongoni pangu kwa jasho, na fikra ilinijia kwa nguvu moja kwa moja toka mahali pa ndani ya utotoni mwangu.

*Ningehitaji poda ya ulanga.*

Tulipokuwa watoto na tulitokwa na jasho, tulirashiwa poda ya ulanga. Ukihalifu, kwa sababu ulidhani umekuwa mno kwa ile poda ya ulanga, utaambiwa ungaliweza kuumwa na ugonjwa wa kifua. Ukiuliza ugonjwa wa kifua ni ugonjwa gani, utaambiwa ni *ugonjwa mbaya*. Na walisema kwa sauti iliyokuhofisha kuuliza tena.

Nikiwaza nilitambua kwamba ilikuwa mara ya pili katika siku mbili fikra za utotoni zilinijia. Ilikuwa sio ya kawaida kwa sababu sikuzoea kabisa kufikiria utoto. nilikuwa sijakumbuka kitu. Kama mtu alipokuwa ameniuliza utoto wangu ulikuwaje, nilimjibu kwa bahati. Mara chache tu nilisema nilikuwa na utoto mzuri na pengine kwamba nilikuwa mtoto mwenye majonzi. Na mara kwa mara nilipotaka kupenya moyoni nilikuwa nimejibu nilikuwa mtoto asiye wa kawaida. Nilikuwa nimefikiri kwamba ningekuwa wa kuvutia zaidi. Sisi watu wenye majaliwa ya peke yake, mara nyingi tulikuwa watoto wasio wa kawaida. Ilikuwa isiyoandikwa lakini rahisi kufahamiwa.

Kwa kweli sijakumbuka mambo yaliyohusiana na utoto wangu na sikuwa na tamaa ya kuyafikiria. Mara kwa mara nimekaza fikira ili

nikumbuke lakini nilidhofika. Basi niliacha. Majonzi siyapendi, afadhali yatahadariwe.

Sasa niliitazama nimeduwaa vipande hivi vya makumbuko yaliyokuwa yakitoka sijui wapi. Yamenipatia huzuni kidogo pamoja na mshangao na uchunguzi. Lakini sikuhisi majonzi, yale ambayo kabla yamenifanya nisiangalie.

Niliwaza badili lile na mwili wangu mzima wamenitapa. ingawa ilikuwa joto sana.

Na ile sigara mi niliiwasha.

Nilimwona Abdou kwa mbali huku akija toka ukumbini.

Alinijia na alinisalimu kwa salamu ya mkono akiinamia kichwa chake pia. Nilimsalimu hivi hivi lakini, baadae, nilizuzuka kidogo.

Alikuwa akishika gazeti mkononi na alisogea pembeni ili niweze kuingia majilisini.

Tuliketi na sote wawili tukiepuka kochi iliyovunjika iliyokuwa kule tangu zamani. Abdou alinipa gazeti akitabasamu.

"Nini?". Niliuliza.

"Wameandika kuhusu yako". Sauti yake imebadilika sasa.

Nilichukua lile gazeti. Lilichapishwa juzi. Labari zilizotolewa zilikuwa kuhusu baraza la Jumanne lililopita na ilikwemo pia picha yangu. Bado sijalisoma wala sijaliona yaani tangu mwaka jana bado sijaanza kununua tena magazeti.

## SHAHIDI MKUU ANAWAYAWAYA MASHTAKANI KWA MAUTI YA MTOTO JINA LAKE FRANCESCO

Jana baraza lilikuwa la tamthilia katika mashtaka juu ya Msenegali Abdou Thiam aliyeshtakiwa kwa kumnyang'anya Francesco Rubino na kumwua. Wamesikilizwa mashahidi wengi na wakuu walioitwa na Mwendesha mashtaka. Mmoja wao ni Mzee Antonio Renna ambaye ni mwenye baa inayokuwepo Capitolo, yaani mtaa ulioko karibu na bahari mjini Monopoli, mahali mtoto alikotoweka.

Wakati wa upelelezi wa kwanza, Mzee Renna alikuwa amesema kwamba alimwona mshtakiwa huku alikuwa akipita mbele ya baa yake, karibu sana na mahali pa kutoweka kwa mtoto, hasa muda mfupi sana kabla ya kutoweka kwenyewe. Shahidi huyu aliyejadiliwa na Mwendesha mashtaka barazani, aliimarisha maneno yake, akijionyesha mwenye yakini kubwa.



Kichocho kilitokea wakati wa maulizo ya ajabu yaliyoendeshwa na mtetezi wa Msenegali, yaani Mzee Guido Guerrieri. Baada ya kutoa maswali mengi ambayo, mwanzoni, yalionekana kama yasiyoleta maovu. Baadaye, kila mtu aliyesikiliza majibu yaliyotolewa na Mzee Renna aliweza kujua kwamba bwana huyu anawachukia sana watu wanaotoka nchi za kigeni, hasa Waafrika. Mtetezi jina lake Guerrieri alimwonyesha picha za watu weusi akimwuliza kama yuko mmoja ambaye yeye anamjua. Mwenye baa wa Capitolo alisema 'hapana', na hapo ndipo mtetezi alicheza karata yake ya muhimu zaidi: picha mbili zilionyesha sura ya mshtakiwa Abdou Thiam. Yaani yule ambaye shahidi Renna alikuwa amesema kwa yakini anamjua sana na kumwona mbele ya baa yake ile siku ya kusikitisha, baada ya mchana. Zile picha zilichukuliwa na watu wa korti kama ushuhuda.

Mwendesha mashtaka Cervellati alijisikia amelazimishwa kumhoji tena yule shahidi kwa kueleza wazi na moja kwa moja habari zote alizozipatia. Yule shahidi alieleza wazi akisema kwamba hajamwona tena mshtakiwa tangu mwaka jana, yaani wakati mambo yote yalipotokea, kwamba hana shaka lolote kuhusu maneno aliyoyasema. Yeye hakuitambua kabisa sura yake mshtakiwa iliyo kwenye picha kwa sababu muda mrefu umeshapita na kwa namna ya picha zile. Kwa kweli zile zilikuwa nakili zenye rangirangi lakini zisizooneka.

Maulizo yaliyoendeshwa na Mwendesha mashtaka yalikuwa safi lakini, bila shaka lo lote, wakati wabaraza hilo mtetezi Guerrieri ametia ishara kwa ajili yake. Hasa katika mashtaka yasiyo rahisi kwamtetezi.

Kabla ya mwenyeji baa, waliulizwa daktari wa kisheria na jemadari Lorusso, yaani mpelelezi aliyeendeshwa uchunguzi.

Maulizo ya jemadari pia yasiyorahisi na yenye mahangaiko wakati ambapo mtetezi alisema kwamba upelelezi ulikuwa umeendeshwa kwa purukushani hasa nyumbani mwa Msenegali.

Leo asubuhi, mashtaka yameendelea na watasikilizwa wazazi wake marehemu mtoto, babu na bibi wake. Jumatatu ijayo, mshtakiwa atasikilizwa na baadaye, kama hayatatolewa maombi mapya ya ushahidi, mateteo yataanzishwa.

Nilisoma nakala ile mara mbili. *Maulizo ya ajabu*. Nilishindwa kuzuia ile furaha ya kitoto niliyokuwa nayo niliposoma maneno yale na kuiona picha yangu kwenye gazeti. Wakati wa maishani mwangu ilikwisha tokea wanagazeti waandike jina langu na waweke picha yangu kwenye gazeti.

Lakini sasa ilikuwa tofauti. Mimi nilikuwa mkuu katika nakala hii.

Nilipigwa picha lini? Ile ilikuwa picha ya zamani kidogo, labda ya miaka miwili iliyopita, lakini sikukumbuka lini. Katika picha ile

nilionekana kama mzuri, lakini mimi binafsi yangu mzuri zaidi, nilifikiri.

Hivyo ndivyo mi niliwaza lakini baada ya sekunde chache tu nilijisikia kama mpumbavu, niliweka lile gazeti meazani na nilimgeukia Abdou.

Alinitazama. Alikuwa na uso wa mtu anaye hakika tutashinda. Alikuwa amesoma gazeti na sasa anafikiri kwamba ni mtu mwenye bahati na anaweza kunitegemea kwa sababu mi mtetezi mwaminifu. Nilijiuliza kama ilkuwa afadhali nimtie ghairi na kumwambia kwamba ingawa mambo yalikuwa mazuri kwa baraza lile, kwa kweli bado uwezekano wa kushinda kabisa ulikuwa mbali. Nilijibu moyoni mwangu afadhali ninyamaze tu. Kwa hiyo nilikonyeza kwa kichwa, nikikunja mabega kidogo. Na yale makonyezo yangu yalikuwa na maana nyingi.

"Sawa Abdou. Sasa lazima tushughulikie baraza lijalo. Hasa utakapoulizwa wewe".

Alikubali kwa kichwa na hakusema neno. Alikuwa mwekevu tu lakini hakusema neno. Lazima niseme mimi.

"Sasa nitakueleza itaendeleaje, na jinsi ambavyo lazima ufanye wewe. Kama hutaelewa nitakachokuambia, tafadhali nikatize na uniambie mara moja".

Alikubali tena kwa kichwa na kwa uthabiti.

"Mwanzoni utajadiliwa na Mwendesha mashtaka. Wakati ambapo atakuuliza, lazima umwangalie usoni. Kwa makini sio kwa ufidhuli. Usimjibu kabla hajamaliza kutoa swali. Atakapomaliza uwageukie mahakimu na uongee nao. Usibishane kabisa na Mwendesha mashtaka. Sawa?".

"Wakati Mwendesha mashtaka anaposema, ni lazima nimwangalie usoni, nitakaposema mimi, lazima niwaangalie mahakimu".

"*Ok*. Utafanya vile vile utakapoulizwa na wakili wa jamii au nami. Lazima uwafahamishe mahakimu kwamba unayasikiliza maswali na unajibu taratibu.. Sawa?".

"Ndiyo".

"Kabla ya kujibu lazima usubiri maswali yamalizike. Hasa nitakapohoji mimi mwenyewe. Lakini, jambo la muhimu sana, lazima wengine wasidhani sisi wakuu wamchezo wa kuigiza, tukisema maneno tuliyojifunza kwa moyo. Umeelewa maana yangu?".

"Ndio, lazima tusionekane kama kucheza kinyago".

"Sawa. Usiketi katika pambizo la kiti. Keti vizuri, hivi. – Nilimwonyesha jinsi ya kuketi kitini vizuri. – Lakini sio hivyo".



Nilimwonyesha tena. Yaani lazima aketi kitini kama mtu mtulivu atavyoketi, yaani kwa raha, bila shida, akitekanya miguu na kadhalika.

"Sawa? Lazima wasifikiri wewe mmoja anayetaka kukimbia, kwa jinsi unavyoketi kitini, lakini lazima pia wasifikiri wewe mtu mwenye raha kabisa. Wanashindana kwa maneno kuhusu maisha yako, kuhusu uwezekano wa kukufunga gerezani kwa miaka mingi, kwa hiyo huwezi kuwa na raha. Ukionekana mwenye raha maana yake ni kwamba unaigiza na wao watanabihi. Laiti bila ufahamu, lakini watanabihi. Unanielewa?".

"Ndiyo".

"Kama hutaielewa maana ya swali, au huna hakika umeifahamu, usijaribu kujibu. Mwombee yule anayekuhoji aseme tena".

"Sawa".

"Basi, kabla ya kuendelea, tafadhali sema tena yote niliyokuambia, tangu mwanzoni mpaka sasa".

"Lazima nimwangalie usoni kila mtu atakayenihoji. Swali litakapomalizika, nigeuke niwaangalie watu wa korti na nijibu. Kama sitaelewa vizuri swali, lazima niombe waseme tena, tafadhali. Lazima niketi hivyo".

"Aliketi kwa jinsi nilivyomwambia mimi. Nilitabasamu na nilikubali kwa kichwa. Alikuwa mtu asiyehitaji mambo yamrudishiwe mara mbili.

Hapo ndipo, toka mfukoni nilitoa nakili ya maulizo yake yaliyofanywa mbele ya Mwendesha mashtaka, na hati nyingine. Baada ya kuelewa jinsi atakavyotenda yeye, ilitubidi tupatane kuhusu mambo atakayosema na jinsi ya kueleza vizuri yale yaliyohadithiwa naye na kuhusu maombi ya mathubuti nitakayouliza baada ya hoji yake.

Nilibaki gerezani mpaka saa tisa baada ya mchana, na hali ya hewa ilizidi kuwa ya joto kali kabisa. Nilipotaka kuondoka tulipeana mkono na mimi nilifikiri kwamba tulikuwa tumepanga yote yaliyowezekana.

Nilienda nyumbani, nilioga, nilivaa suruali nyepesi na shati. Halafu nilitayarisha saladi, nilikula, nimeketi kochini, nilivuta sigara mbili huku nikinywa kahawa ya kimarekani iliyosukwa. Kuelekea saa kumi na nusu nilitoka kwa kwenda ofisini. Nilijaribu kumwita Margherita lakini hakuwamo nyumbani. Nilisikitika kidogo na nilifikiri nitamwita tena baadaye, yaani baada ya kazi.

Ofisini, nilipokea mteja wangu fulani, alinipitia karani wangu wa hesabu, nilizisoma barua na, mwishoni nilimwambia Maria Teresa kwamba siku ile anaweza kuondoka mapema. Niliangua macho yangu

nikitazama karatasi ilyokuwa mezani. Nilipotazama tena niliona bado hajaondoka, alisimama tu. Nilimwangalia kwa kicheko cha kuuliza. Alikuwa msichana sio mzuri sana, lakini macho yake yenye rangi ya sawati yalikuwa mazuri sana na tena makali sana. Alikuwa akifanya kazi kwangu tangu miaka minne na pale pale anajaribu kupata digrii ya elimu ya kisheria katika Chuo Kikuu. Alitamani kuwa jaji.

"Kuna nini?", niliuliza kwa kicheko kile changu cha kuuliza. Yeye alionekana anatafuta maneno.

"Lazima nikuambie kwamba nimefurahi... nimefurahi umepona. Nilikuwa na...wasiwasi kubwa".

Nilishindwa kusema lo lote. Tangu tulipojuana bado hatujawahi kuzungumza kuhusu mambo yetu. Baada ya miaka minne bado sijajua ana mchumba au sio, anafikiri nini na kadhalika. Kwa kweli, sikufikiri atasema maneno kama yale, ingawa nilijua sana moyoni mwangu kwamba alikuwa ametambua hali yangu. Alianza kusema tena.

"Ningalitaka kukusaidia, ulipokuwa vibaya, lakini wewe ulikuwa wa mbali sana. Nilikuwa na wasiwasi na fikra mbaya sana zilinijia kichwani".

"Fikra mbaya?".

"Ndiyo, usicheke tafadhali. Niliwafikiria wale wanaojiua na baadaye marafiki wao na majirani wanasema kwamba wale walikuwa na huzuni na kwamba walionekana wamebadili hali yao, na mambo kama haya...".

"Ulifikiri nitaweza kujiua?".

"Ndio. Lakini tangu muda fulani mambo yameanza kubadilika kidogo na mi nilikuwa nimefurahi sana. Sasa naona yanaendelea vizuri zaidi na nilipenda kukuambia kwamba nimefurahi".

Sikujua nimjibu nini. Maneno yasiyo na maana tu yale yaliyonijia mdomoni na mi sikutaka kuyasema. Nilifikiri kwamba mara nyingi tunakaribiana na watu wa ajabu na hatujawaona kabisa. Nilihangaika tu.

"Asante", nilisema. Lakini, mara nilisimama, nilimkaribia na nilimpa busu usoni. Aliona haya kidogo.

"Basi... tutaonana Jumatatu".

"Haya, Jumatatu. Asante, Maria Teresa".

Lazima nimalize tayarisho langu kwa maulizo ya Abdou na ilinibidi nielewe mambo fulani kuhusu jinsi ya kufanya maombi yangu na ushahidi wa nyongeza. Kwa hiyo nilibaki kufanya kazi mpaka saa mbili usiku, kisha nilifunga kila kitu na nilitoka. Nje, anga la mwisho la jua lilikuwa



liking'aa na hali ya hewa ilikuwa ya baridi kidogo. Ilikuwa safi na mimi nilifurahi sana. Nilikuwa nimefanya kazi yangu, ulikuwa wakati wa jua kali na tena Ijumaa. Tangu zamani, kwa mara ya kwanza niliona kwamba wikiendi ilikuwana maana yake, na maono yale yalikuwa mazuri sana. Nilipenda kufanya kitu fulani ili nisherehekee mimi binafsi.

Nilijaribu kumpigia simu Margherita kwa simu ya mkononi, lakini bure. Nilijaribu kumwita nyumbani lakini hakuwamo. Nilisikitika kidogo, lakini kidogo tu.

Nilifikiri ningependa kufanya nini na jibu limenijia mapema. Kwa hiyo nilienda nyumbani, nilitayarisha mzigo mdogo, nilichukua vitabu fulani, nilipanda garini na nilienda kuelekea upande wa kusini. Yaani pwani.

Nilifika kijijini pa Santa Maria di Leuca kama saa tano usiku na nilipanga chumba katika pensheni iliyokuwa karibu na bahari. Nilienda kula chakula cha jioni na baadaye nilitembeatembea karibu na pwani, nikiketi mara kwa mara ufungani pafupi kwa kuvuta sigara wakati niliwaangalia watu na kupendezwa na baridi ya usiku. Nilienda kulala kama saa saba na nusu. Nilitikita usingizi na niliamka saa tatu asubuhi ya Jumamosi. Nilifikiri kwamba sikukumbuka tangu sijawahi kulala hivyo. Labda nilizoea kulala hivyo nilipokuwa namiaka ishirini tu, au baadaye kidogo.

Nilitumia siku mbili hizo kwa kupendezwa na bahari, jua kali, kusoma na kuwaangalia watu. Kufikiri sikufikiri. Wakati wa jioni niliwaangalia watu waliokuwa pwani, hotelini, njiani pa kijiji. Nilitumia masaa yote nikiwaangalia watu, sikujali kabisa wakiniangalia na kunifahamu. Pwani, Jumamosi asubuhi nilifanya urafiki na mama mmoja aliyetoka mjini Lecce. Alikuwa kama mwenye umri wa miaka sitini na tano, na mnene. Alivaa mavazi ya bahari yenye maua ya rangi ya samawati. Alikuwa wa kupendeza na alinisimulia kwamba mume wake alikuwa amefariki miaka mitatu iliyopita na kwamba yeye alikuwa amesikitika sana kwa miezi mitano au sita na alifikiri maisha yake pia yamemalizika kwa sababu walioana alipokuwa na miaka ishirini na mbili na yule mume wake alikuwa mtu wake wa kwanza na wa pekee. Kisha, alikuwa ameanza kufikiri kwamba maisha yake labda hajamalizika na kwamba yalibaki mambo fulani aliyoyapenda kufanya walakini, na kwa sababu mbalimbali, aliyachelewesha. Kwa hiyo alifuata mfulizo wa masomo ya 'origami' iliyokuwa katika vitu alivyotaka kuvifanya. Kwa sababu, alipokuwa mtoto bibi yake alimtengenezea vititia vizuri sana akiikunja karatasi, na